# MKAKATI WA TAIFA DHIDI YA RUSHWA NA MPANGO WA UTEKELEZAJI AWAMU YA TATU 2017-2022

**Ofisi ya Rais,**
**Ikulu,**
**Dar es Salaam, Tanzania**

**JULAI, 2017**

# Yaliyomo


**VIFUPISHO VYA MANENO** ........................................ viii
**UTANGULIZI** ........................................ xi
**DIBAJI** ........................................ xv

**SURA YA KWANZA** ........................................ 1
MUKTADHA WA MAPAMBANO DHIDI YA RUSHWA TANZANIA ........................................ 1
1.0 Chimbuko ........................................ 1
1.1 Hali ya Rushwa ........................................ 3

**SURA YA PILI** ........................................ 5
MKAKATI WA TAIFA DHIDI YA RUSHWA NA MPANGO WA UTEKELEZAJI AWAMU YA KWANZA NA YA PILI ........................................ 5
2.0 Utangulizi ........................................ 5
2.1 Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji Awamu ya I na II ........................................ 6
2.2 Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji Awamu ya Kwanza ........................................ 9
2.2.1 Mafanikio ........................................ 9
2.2.2 Changamoto ........................................ 9
2.3 Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji Awamu ya Pili ........................................ 12
2.3.1 Malengo ya Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji Awamu ya Pili ........................................ 14
2.3.2 Mfumo wa Sheria na Kitaasisi ........................................ 15

2.3.3 Muundo wa Utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji Awamu ya Pili ........................................ 18
2.3.4 Jitihada zingine zilizotekelezwa sanjari na Mkakati wa Taifa dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji Awamu ya Pili ............................ 19
2.3.5 Mafanikio na Changamoto za Utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Pili ........................................................................ 21

**SURA YA TATU** ........................................................ 25
MKAKATI WA TAIFA DHIDI YA RUSHWA NA MPANGO WA UTEKELEZAJI AWAMU YA TATU ......... 25

3.0 Utangulizi ........................................................ 25
3.1 Lengo Kuu la Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji Awamu ya Tatu ........................ 25
3.2 Nyenzo za Utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji Awamu ya Tatu .... 32
3.2.1 Mipango Kazi ........................................................ 32
3.2.2 Kamati za Kudhibiti Uadilifu .............................. 32
3.2.3 Jukwaa la Kitaifa la Mapambano Dhidi ya Rushwa ........................................................ 32
3.2.4 Kamati ya Taifa ya Uendeshaji ............................ 32
3.2.5 Kamati ya Taifa ya Kitaalam ya Ushauri ........... 32
3.2.6 Uratibu wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji Awamu ya Tatu ...... 32
3.2.7 Ubia na Ushirikiano katika Mapambano Dhidi ya Rushwa na Taasisi za Kitaifa, Kikanda na Kimataifa ........................................................ 35

3.2.8 Programu za Kujenga Uwezo kwa Taasisi Zisizokuwa za Kiserikali ..................................... 35
3.2.9 Mikataba ya Huduma kwa Wateja ..................... 35
3.2.10 Mfumo wa Kushughulikia Malalamiko ........... 36
3.2.11 Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini .................. 36
3.3 Vigezo Muhimu vya Kufanikisha Utekelezaji wa Mkakati .................................................................... 36
3.3.1 Uongozi wa Kimageuzi ....................................... 37
3.3.2 Sera Bora na Malengo yanayopimika ................. 37
3.3.3 Habari, Elimu na Mawasiliano ............................ 37
3.3.4 Kutenganisha Siasa na Shughuli za Utawala ..... 38
3.3.5 Mfumo Madhubuti wa Utoaji wa Haki na Uhuru wa Mahakama ......................................... 39
3.3.6 Upatikanaji wa Rasilimali za Kutosha ............... 39

**SURA YA NNE** .......................................................... 40
MPANGILIO WA KITAASISI NA MAJUKUMU ............. 40
4.0 Utangulizi ................................................................ 40
4.1 Ngazi ya Taifa ............................................................ 41
4.1.1 Majukumu ya Kamati ya Taifa ya Uendeshaji ... 41
4.1.2 Majukumu ya Kamati ya Taifa ya Kitaalam ya Ushauri ................................................................ 42
4.2 Ngazi ya Mkoa ........................................................... 43
4.2.1 Majukumu ya Kamati ya Uratibu ya Mkoa ....... 43
4.3 Ngazi ya Wilaya ........................................................ 44
4.3.1 Majukumu ya Kamati ya Uratibu ya Wilaya ..... 44
4.4 Ngazi ya Kata ............................................................. 45
4.4.1 Majukumu ya Kamati ya Uratibu ya Kata ......... 45
4.5 Ngazi ya Kijiji/Mtaa ................................................. 46

4.5.1 Majukumu ya Kamati ya Uratibu ya Kijiji/ Mtaa .................................................................... 46
4.6 NGAZI YA TAASISI .................................................... 47
4.6.1 Taasisi za Umma .................................................... 47
4.6.1.1 Majukumu ya Taasisi za Umma ............... 47
4.6.2 Taasisi Simamizi za Masuala ya Utawala Bora .. 51
4.6.3 Taasisi Zisizokuwa za Kiserikali ......................... 52

**SURA YA TANO** ............................................................ 56
UFUATILIAJI NA TATHMINI ......................................... 56
5.0 Utangulizi ...................................................................... 56
5.1 Madhumuni ya Mpango wa Ufuatiliaji na Tathmini ..... 57
5.2 Muundo wa Ufuatiliaji na Tathmini ............................... 58
5.3 Mfumo wa Viashiria vya Upimaji Matokeo .................... 58
5.3.1 Mfumo wa Matokeo na Uchaguzi wa Viashiria vya Upimaji ........................................................... 59
5.4 Usambazaji na Matumizi ya Taarifa ............................... 64
5.5 Taarifa kwa Wadau ........................................................ 64
5.6 Utoaji wa Taarifa za Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji Awamu ya Tatu .... 64
5.7 Mchakato wa Utoaji Taarifa .......................................... 65
5.7.1 Vyanzo vya Taarifa ................................................. 65
5.7.2 Taarifa za Utekelezaji za Robo Mwaka ............... 65
5.7.3 Taarifa ya Utekelezaji ya Mwaka ......................... 65
5.7.4 Taarifa ya Tathmini ya Upimaji wa Matokeo ..... 66
5.7.5 Uchambuzi na Uunganishaji wa Takwimu ........ 66
5.7.6 Uidhinishwaji na Usambazaji wa Taarifa ........... 66
5.7.7 Taarifa kwa Wadau ............................................... 67
5.8 Mpangilio wa Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Mkakati wa Awamu ya Tatu ............................................ 67

5.8.1 Uratibu wa Serikali wa utekelezaji wa Mkakati wa Awamu ya Tatu ................................................ 67
5.8.2 Mfumo wa Kanzidata wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji Awamu ya Tatu ........................................................................ 68
5.8.3 Bajeti na Mpango Kazi wa Ufuatiliaji na Tathmini ................................................................. 69

**SURA YA SITA** .......................................................................... 70
MWONGOZO WA UANDAAJI WA MPANGO KAZI WA UTEKELEZAJI WA MKAKATI WA TAIFA DHIDI YA RUSHWA AWAMU YA TATU ....................................... 70
6.0 UTANGULIZI ................................................................... 70
6.1 Mipango Kazi ................................................................... 71
6.2 Lengo na Mikakati ya Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji Awamu ya Tatu .... 72
6.3 Utaratibu wa Kuandaa Mpango Kazi ............................ 73
6.4 Mpango wa Ufuatiliaji na Tathmini ............................... 96
6.4.1 Mpango wa Ufuatiliaji ........................................... 96
6.4.2 Mpango wa Tathmini ............................................ 110
6.5 Muundo wa Kamati za Kudhibiti Uadilifu na Vikao .... 113
6.6 Mpango wa Utoaji wa Taarifa ....................................... 113
6.6.1 Mpango wa Utoaji wa Taarifa za Ndani ............. 113
6.6.2 Mpango wa Utoaji Taarifa nje ............................... 115

## VIFUPISHO VYA MANENO

| | | |
|---|---|---|
| ALAT | - | Association of Local Authorities of Tanzania |
| APRM | - | African Peer Review Mechanism |
| AZAKI | - | Asasi za Kiraia |
| BRELA | - | Business Registration and Licensing Authorities |
| CCM | - | Chama Cha Mapinduzi |
| CoST | - | Construction Sector Transparency Initiative |
| EITI | - | Extractive Industry Transparency Initiative |
| FSRP | - | Financial Sector Reform Program |
| GGCU | - | Good Governance Coordination Unit |
| GPSI | - | General Public Impact Survey |
| IARs | - | Investigative Agencies Reports |
| LGRP | - | Local Government Reform Program |
| LSRP | - | Legal Sector Reform Program |
| MKUKUTA | - | Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania |
| MMM | - | Mtendaji Mkuu wa Mahakama |
| NACSAP | - | National Anti-Corruption Strategy and Action Plan |
| OGP | - | Open Government Partnership |
| OS | - | Outcome Survey |
| PCTS | - | Public Complaints Tracking Systems |
| PFARs | - | Public Finance Accountability Reports |

| | | |
|---|---|---|
| PFMRP | - | Public Financial Management Reform Program Government |
| PPRs | - | Public Procurement Reports |
| PSRP | - | Public Sector Reform Program |
| REPOA | - | Research for Poverty Alleviation |
| TAKUKURU | - | Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa |
| TAKURU | - | Taasisi ya Kupambana na Rushwa |
| TAMISEMI | - | Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| TEHAMA | - | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| THBUB | - | Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora |
| UNDP | - | United Nations Development Program |

# UTANGULIZI

Serikali ya Tanzania imekuwa ikisisitiza kuwa Utawala Bora ni kipaumbele cha kufikia malengo ya Maendeleo ya Taifa. Utawala Bora umekuwa ni jambo muhimu katika kukuza na kuimarisha amani na utulivu, ukuaji wa uchumi, ustawi wa jamii na kupunguza umaskini hapa nchini. Utawala Bora umesisitizwa na kuimarishwa katika sekta muhimu kwa kutekeleza maboresho mbalimbali katika Sekta ya Umma. Maboresho hayo ni Programu ya Maboresho katika Utumishi wa Umma, Usimamizi wa Fedha za Umma, Sekta ya Sheria, Serikali za Mitaa na Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji.

Pamoja na maboresho haya, programu katika sekta zingine zimetekelezwa ili kuimarisha utoaji wa huduma na kuzuia na kupambana na rushwa.

Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji ulikuwa ni moja ya maboresho ya Sekta ya Umma ambao ulitekelezwa katika awamu mbili, awamu ya kwanza na ya pili (2001 -2011). Matokeo ya utekelezaji wa Mkakati huu ni kuanzishwa kwa mfumo wa ukuzaji wa uwajibikaji, uwazi na uadilifu katika matumizi ya rasilimali za umma kwa lengo la kuimarisha utoaji wa huduma na ustawi wa wananchi.

Hivyo basi, Awamu ya Tatu ya Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa ni muendelezo wa juhudi za Serikali za kuunga mkono mapambano dhidi ya rushwa ili kuimarisha utawala bora katika sekta zote za uchumi. Mkakati umeandaliwa ili kuendeleza na kuimarisha mafanikio yaliyofikiwa na hatua zilizochukuliwa ili kutatua changamoto zilizojitokeza katika afua zilizochukuliwa. Mkakati umelenga zaidi katika mfumo wa ugatuaji ambapo ngazi mbalimbali za Serikali zitashiriki kikamilifu katika hatua za utekelezaji. Aidha, Mkakati umeimarisha Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini ambao utasaidia kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa Mkakati. Vilevile, Mkakati umeandaliwa kwa kuhusisha wadau wengi zaidi wakiwemo Wadau wa Maendeleo, Jumuiya za Kiraia, Sekta Binafsi, Vyombo vya Habari, Taasisi za Dini, Vyama vya Kitaaluma, Vyama vya Siasa, na Sekta ya Umma kwa ujumla.

Kama ilivyoelezwa hapo awali, Awamu ya Tatu ya Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa imeandaliwa ikiwa na mtizamo mpya unaolenga kuhakikisha kuwa rushwa inaondolewa kabisa Nchini kwa kutumia mbinu mpya na zinazotekelezeka za kuzuia na kupambana na rushwa kwa kuweka mkazo katika sekta zenye mazingira shawishi ya rushwa. Msisitizo zaidi utawekwa kwenye Sekta za kimkakati za ukusanyaji wa mapato, uvunaji na matumizi

ya maliasili, mafuta na gesi na maeneo mengine yote ya uchumi yenye ushawishi zaidi wa vitendo vya rushwa.

Hivyo basi, malengo mahsusi ya Awamu ya Tatu ya Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa ni:

(i) Kuimarisha ufanisi, uwazi na uwajibikaji wa utoaji wa huduma katika Sekta ya Umma na Binafsi;

(ii) Kutekeleza kwa ufanisi Mikakati ya mapambano dhidi ya rushwa;

(iii) Kuzijengea uwezo Taasisi Simamizi za mapambano dhidi ya rushwa; na

(iv) Kuwa na uongozi madhubuti wa kisiasa katika mapambano dhidi ya rushwa.

Kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, natoa rai kwa wananchi na wadau wengine kuendelea kufanya kazi kwa karibu na Serikali wakati wa utekelezaji wa Awamu ya Tatu ya Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa, hususan mabadiliko ya fikra na kushiriki kikamilifu ili kuhakikisha kuwa malengo ya Awamu ya Tatu ya Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa yanafikiwa.



*Angellah Jasmine Kairuki (MB)*
**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais**
**(Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora)**

# DIBAJI

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatambua kuwa rushwa ni tatizo kubwa linaloathiri maendeleo ya kiuchumi na kijamii, na hivyo imedhamiria kutekeleza Sera ya kutovumilia vitendo vya rushwa katika shughuli zake. Hatua kadhaa za makusudi zimechukuliwa tangu uhuru kushughulikia tatizo hili ikiwemo kuandaa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji ambao ni mfululizo wa jitihada za Serikali katika kukabiliana na rushwa.

Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji ni moja ya hatua madhubuti za Serikali ambao ulitekelezwa kwa awamu mbili katika kipindi cha muongo mmoja (2001 – 2011). Lengo pana la Mkakati huu ni kuboresha/kuimarisha mifumo na mchakato wa kuzuia na kupambana na rushwa. Mkakati ulijielekeza katika kuimarisha na kuendeleza Mifumo ya Uadilifu, Uwazi na Uwajibikaji katika Taasisi za Umma.

Utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji Awamu ya Kwanza na ya Pili ulitekelezwa sanjari na maboresho yaliyokuwa yakitekelezwa katika Sekta ya Umma. Utekelezaji wa Mkakati katika awamu hizo mbili ulikuwa na manufaa yaliyoambatana na changamoto. Changamoto hizo na

matokeo ya tathmini ya utekelezaji wa awamu hizo mbili, zimetumika kama fursa katika maandalizi ya Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji Awamu ya Tatu (National Anti-Corruption Strategy and Action Plan-NACSAP III).

Maandalizi ya Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji Awamu ya Tatu yameshirikisha wadau kutoka Sekta ya Umma na Binafsi. Serikali iliunda kikosi kazi kilichojumuisha wajumbe kutoka Taasisi Simamizi za masuala ya Utawala Bora ili kukamilisha kazi hii. Wajumbe hao walitoka Ofisi ya Rais, Ikulu; TAKUKURU; Ofisi ya Makamu wa Rais; Ofisi ya Waziri Mkuu; Ofisi ya Rais – TAMISEMI; Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma; Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora; Mamlaka ya Manunuzi ya Umma; Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Wizara ya Mambo ya Katiba na Sheria.

Utekelezaji wa Mkakati wa Awamu ya Tatu unalenga kupunguza na kudhibiti rushwa katika Sekta/maeneo muhimu ya kimkakati ambayo ni pamoja na **manunuzi ya umma, ukusanyaji wa mapato, utoaji wa haki, maliasili na utalii, madini, nishati, mafuta na gesi, afya, elimu na ardhi**. Kipaumbele kitatolewa kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania, Polisi, Mahakama, Mamlaka ya Bandari Tanzania, Afya, Elimu, Michakato ya kibiashara na

Mahusiano ya kitaasisi. Hivyo, lengo kuu la Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji Awamu ya Tatu ni kuhakikisha rushwa inapungua kwa kiasi kikubwa nchini kupitia hatua za kuzuia na kupambana na rushwa. Malengo mahsusi yatakayowezesha kufikiwa kwa matokeo tarajiwa ni kama ifuatavyo:

(i) Kuimarisha ufanisi, uwazi na uwajibikaji wa utoaji wa huduma katika sekta ya umma na binafsi;
(ii) Kuwa na ufanisi katika utekelezaji wa mikakati ya mapambano dhidi ya rushwa;
(iii) Kuzijengea uwezo taasisi simamizi za mapambano dhidi ya rushwa; na
(iv) Kuwa na uongozi madhubuti wa kisiasa unaoshiriki kwa dhati katika mapambano dhidi ya rushwa.

Uratibu wa utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Tatu utafanyika ndani ya muundo wa Serikali uliopo kuanzia ngazi ya Kijiji/Mtaa hadi Taifa kupitia **Kamati za Kudhibiti Uadilifu na Kamati za Uratibu wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa.** Kamati hizi zitajenga na kuimarisha umiliki wa Mkakati na uwajibikaji wa viongozi na watendaji katika kuimarisha utawala bora na mapambano dhidi ya rushwa. Kamati zinatarajiwa kushiriki ipasavyo katika uratibu wa

utekelezaji wa Mkakati ili kuwezesha kufikiwa kwa malengo yaliyopangwa. Ufanikishaji wa malengo ya Mkakati wa Awamu ya Tatu utategemea utendaji mzuri wa Kamati husika katika ngazi zote.

Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini utakuwa ni chombo muhimu sana katika utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Tatu. Mfumo huo utatekelezwa kupitia Mpango wa Ufuatiliaji utakaoandaliwa kwa lengo la kurasimisha shughuli zake. Mfumo utatumika kupima matokeo ya utekelezaji wa Mkakati wa Awamu ya Tatu katika kuzuia na kupambana na rushwa katika ngazi mbalimbali, zikiwemo zifuatazo: Kamati ya Taifa ya Uendeshaji, Kamati ya Taifa ya Kitaalam ya Ushauri, Kitengo cha Uratibu wa Utawala Bora- Ikulu; Kamati za Uratibu wa Mkakati ngazi ya Mkoa, Wilaya, Kata na Kijiji/Mtaa na Kamati za Kudhibiti Uadilifu na Kamati za Menejimenti /Uongozi katika Sekta za Umma. Hivyo, kila mtekelezaji wa Mkakati atapaswa kuandaa na kutekeleza Mpango wake wa ufuatiliaji na tathmini, kuandaa na kusambaza kwa mamlaka husika taarifa za utekelezaji wa Mkakati kwa vipindi vya robo mwaka na mwaka mmoja.

Utekelezaji wa Mkakati utazingatia malengo yaliyomo katika Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17-2020/21), Ilani

ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015 na Hotuba ya Ufunguzi wa Bunge la Kumi na Moja la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliyotolewa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 20 Novemba, 2015, mjini Dodoma. Aidha, Sheria za mapambano dhidi ya rushwa zitatungwa au kuhuishwa kwa lengo la kuwa na Sheria madhubuti zitakazoimarisha utawala bora nchini.

Lengo la Serikali ni kuhakikisha kuwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi yanafikiwa kwa kuzingatia misingi ya uwazi na uwajibikaji. Hivyo, kwa kuhitimisha ninarudia kusisitiza kwa Viongozi wa Serikali katika ngazi zote, AZAKI, Sekta Binafsi na Wananchi kwa ujumla wote washiriki katika kufuatilia kwa ukaribu utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji Awamu ya Tatu katika Taasisi zao na Taifa kwa ujumla.

Tutekeleze Mkakati wa Taifa dhidi ya Rushwa – Awamu ya Tatu kwa ajili ya Maendeleo na Ustawi wa Taifa Letu.

*Balozi Mha.* **John W.H. Kijazi**
**KATIBU MKUU KIONGOZI**

# SURA YA KWANZA

# MUKTADHA WA MAPAMBANO DHIDI YA RUSHWA TANZANIA

## 1.0 Chimbuko

Kitendo cha rushwa kinatafsiriwa kuwa ni kuahidi, kutoa, kupokea au kushawishi moja kwa moja au kupitia wakala, kitu chochote cha thamani ili kupindisha utaratibu katika utoaji wa maamuzi. Rushwa ni janga ambalo lina athari hasi katika jamii. Inadhoofisha ustawi wa demokrasia katika nchi; ukiukwaji wa haki za binadamu; inaharibu mfumo wa masoko; inasababisha mmomonyoko wa maadili katika jamii; inachelewesha maendeleo ya nchi; inaruhusu uhalifu wa kupangwa, ugaidi na vitisho vingine vinavyotishia ustawi na usalama wa raia.

Rushwa inaathiri wananchi kwa kuchepusha rasilimali zilizotengwa kwa ajili ya maendeleo, inadhoofisha uwezo wa Serikali wa kutoa huduma za msingi, kukosekana kwa usawa na haki na kukatisha tamaa watoa misaada wa nje na uwekezaji. Kwa njia moja au nyingine, rushwa huhusiana na udanganyifu ambao unahusisha kutotimiza wajibu, kujitambulisha kwa uongo au jaribio la kupotosha ukweli ili kujipatia faida ya fedha au manufaa mengineyo. Kwa hiyo, rushwa na udanganyifu huathiri maendeleo ya uchumi wa nchi na ni kikwazo kikubwa katika kupunguza umaskini na kukuza maendeleo.

Pamoja na Serikali kuwa na Sera ya Kutovumilia Vitendo vya Rushwa, tatizo hili limeendelea kuathiri Sekta za

Umma na Binafsi. Hivyo, kwa miaka mingi Serikali imeendelea na mapambano dhidi ya rushwa kwa kuwa na Sera, Sheria na kuchukua hatua za kiutawala. Kutayarishwa kwa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji wake Awamu ya Kwanza (2001 – 2005) na Awamu ya Pili (2006 – 2011) ni hatua mbili muhimu za awali zilizochukuliwa na Serikali katika kuzuia na kupambana na rushwa nchini.

Maandalizi ya Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji ni matokeo ya uchunguzi uliofanywa na Tume ya Rais ya Kero za Rushwa (Warioba Ripoti ya 1996). Tume iliundwa na kupewa jukumu la kubaini ukubwa wa tatizo la rushwa na kutoa mapendekezo ya namna ya kukabiliana na tatizo hilo.

Hatua nyingine zilizochukuliwa na Serikali katika kukuza utawala bora, kuzuia na kupambana na rushwa ni pamoja na kutekelezwa kwa maboresho katika Sekta ya Umma, Nchi kujiunga na Mpango wa Nchi za Kiafrika kuhusu Kujitathmini katika nyanja za utawala bora na mapambano dhidi ya rushwa (APRM), Mpango wa Kuendesha Shughuli za Serikali kwa Uwazi (OGP), Uwazi wa Mikataba na Taarifa za Madini (EITI) na Mpango wa Kuongeza Uwazi katika Sekta ya Ujenzi (CoST).

Sanjari na jitihada hizo, Serikali imesimamia kutungwa kwa Sheria muhimu ikiwemo Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Sura ya 329, Sheria ya Manunuzi ya Umma, Sura ya 410, Sheria ya Kutakatisha Fedha, Sura ya 256 na Sheria ya Gharama za Uchaguzi, Sura ya 343.

### 1.1 Hali ya Rushwa

Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji wake pamoja na mipango mingine ya mapambano dhidi ya rushwa imetekelezwa kwa zaidi ya muongo mmoja na imesaidia katika kuboresha utawala bora nchini. Hizi ni hatua za ndani zinazochukuliwa katika kuzuia na kupambana na rushwa nchini. Kama sehemu ya utekelezaji wa Mkakati Awamu ya Pili, Kamati za Kudhibiti Uadilifu zilianzishwa katika kila Taasisi ya Umma kwa lengo la kuratibu utekelezaji wa Mkakati.

Hata hivyo, taarifa za viashiria vya utawala bora zilizotolewa na watafiti wakiwemo "***MO Ibrahim***" na "***Transparency International***" zimeonesha kuwa Serikali ya Tanzania imepiga hatua kubwa katika kuimarisha utawala bora. Utafiti wa "***MO Ibrahim***" kuhusiana na masuala ya utawala bora wa mwaka 2012, umebainisha kuwa Tanzania imeshika nafasi ya pili kwa kuwa na kiwango kidogo cha rushwa kwa Nchi za Afrika Mashariki.

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa (NACSAP), udhaifu wa Sheria na usimamizi wake, udhaifu wa mifumo ya ufuatiliaji na tathmini, na udhaifu katika uratibu vimetajwa kuwa ni miongoni mwa changamoto za utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji.

Changamoto hizo zimeongeza malalamiko ya umma dhidi ya vitendo vya rushwa katika Sekta ya Umma kama ilivyoripotiwa kwenye **Taarifa ya Utafiti wa Hali ya Rushwa na Utawala Bora (2009), Viashiria vya Ndani vya Upimaji wa Rushwa na Jitihada za Mapambano Dhidi ya Rushwa (2015), Tathmini ya Utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji Awamu ya Pili (2011) na Taarifa ya mwaka 2014/15 ya utekelezaji wa Mkakati**. Tafiti na taarifa hizi zimebainisha uwepo wa rushwa katika utoaji wa huduma katika Sekta za Mahakama, Polisi, Afya, Elimu, Maliasili, Ukusanyaji wa Mapato, Ardhi na Manunuzi ya Umma.

Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji Awamu ya Tatu unapendekeza kufanyika utafiti zaidi ili kubaini mafanikio na changamoto zinazoathiri jitihada za kuzuia na kupambana na rushwa nchini. Tafiti hizi zitakuwa kielelezo cha kuonesha ni kwa kiwango gani Mkakati na jitihada nyinginezo kama vile kutungwa kwa Sheria na kuanzishwa kwa taasisi zinavyochangia katika kuzuia na kupambana na rushwa nchini Tanzania.

# SURA YA PILI

# MKAKATI WA TAIFA DHIDI YA RUSHWA NA MPANGO WA UTEKELEZAJI AWAMU YA KWANZA NA YA PILI

## 2.0 Utangulizi

Kimsingi inakubalika kuwa utawala bora ni nyenzo muhimu katika ukuaji wa uchumi, ustawi wa jamii, uwekezaji na maendeleo. Sera madhubuti ya Utawala Bora, Sheria na utekelezaji wake ni chachu ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii, utoaji wa haki sawa kwa jamii, na matumizi mazuri ya misaada ya maendeleo kutawasaidia watu na nchi kuondokana na umaskini.

Tangu Uchaguzi Mkuu wa kwanza wa vyama vingi Mwaka 1995, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeweka suala la kuboresha na kuimarisha uchumi kama moja ya vipaumbele vyake vikuu. Katika kufanikisha lengo hili, Serikali imetekeleza maboresho kadhaa katika Sekta ya Umma yakiwemo ulegezaji wa masharti ya kiuchumi, uboreshaji na ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma hasa yale yaliyokuwa yanaendeshwa kwa hasara na jitihada za jumla za Serikali kwa lengo la kuleta ufanisi katika utoaji wa huduma bora kwa umma.

Hata hivyo, jitihada za Serikali zilikwamishwa kwa kushamiri kwa rushwa katika sekta zote za uchumi, siasa na jamii. Athari kubwa zimejitokeza kwenye nyanja za manunuzi ya umma, makusanyo ya mapato yatokanayo

na kodi, ushuru na malipo mengine ya kifedha, ukosefu wa mapato kutokana na mirabaha katika maliasili au gawio katika mali za Serikali. Katika kukabiliana na hali hii, Serikali iliona hapana budi kuchukua hatua kali za kupambana na tatizo hili.

### 2.1 Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji Awamu ya I na II

Tangu awali, Sera ya Serikali ya mapambano dhidi ya rushwa ni ya kutovumilia rushwa na hii inathibitishwa na jitihada mbalimbali za Serikali za kupambamba na rushwa, ikiwemo kuundwa kwa Tume ya Kudumu ya Uchunguzi Mwaka 1966. Lengo kuu la Tume lilikuwa ni kudhibiti matumizi mabaya ya madaraka ya Maofisa wa Serikali na Wakala zake.

Hii ilifuatiwa na kuanzishwa kwa Kikosi cha Kuzuia Rushwa Mwaka 1975 baada ya Bunge kupitisha Sheria ya Kuzuia Rushwa Na. 16 ya 1971, kuundwa kwa Kamati ya Kusimamia Maadili ya Viongozi wa Umma, kutungwa kwa Sheria ya Maadili Na. 6 ya Mwaka 1973 na kutungwa kwa Sheria ya Uhujumu Uchumi ya Mwaka 1984 iliyounganisha makosa ya rushwa kuwa makosa ya uhujumu uchumi.

Aidha, Ilani ya Uchaguzi ya Mwaka 1995 ya Chama Tawala, [Chama Cha Mapinduzi (CCM)], ilionesha nia ya kupambana na rushwa.  Baada ya Uchaguzi Mkuu, Serikali ilianzisha hatua kadhaa za Kisera na Kisheria

zilizodhamiria kukabiliana na tatizo la rushwa. Hatua hizo ni pamoja na kutungwa kwa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Na. 13 ya Mwaka 1995 na kuundwa kwa Tume ya Rais ya Kero za Rushwa (PCIAC) iliyofanya utafiti kuhusu vyanzo vya rushwa. Taarifa ya Tume hiyo ya Mwaka 1996 ilibaini njia kuu mbili za namna rushwa inavyoweza kujidhihirisha nchini ambazo ni:

**(a) Rushwa katika Mifumo ya Utawala (Rushwa Ndogo)**

Hii ilihusisha zaidi watumishi wa Serikali na mawakala wao kudai rushwa kwa wananchi kwa huduma zinazotolewa bure. Taarifa hiyo imeeleza kuwa aina hiyo ya rushwa uchwara inasababishwa na viwango vidogo vya mishahara vinavyotolewa kwa wafanyakazi ambavyo havikidhi mahitaji.

**(b) Rushwa Kabambe (Kubwa)**

Aina hii ya rushwa imebainishwa kuhusisha Viongozi wa ngazi za juu Serikalini wenye mamlaka ya kutoa maamuzi kupitia Sera na Mikataba. Taarifa hiyo ilibainisha kuwa sababu kubwa ya rushwa hiyo ni ulafi uliokithiri na kujilimbikizia mali.

Taarifa hiyo pia imebainisha kutokuwepo kwa uwazi na uwajibikaji kuwa ni moja ya sababu ya kuwepo rushwa katika Sekta ya Umma. Taarifa imetoa mapendekezo ya kufanya mabadiliko makubwa katika mifumo ikiwemo kuibadilisha Taasisi ya Kuzuia Rushwa (TAKURU) kuwa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa

(TAKUKURU), kuimarishwa kwa Kitengo cha Uratibu wa Utawala Bora-Ikulu, kuanzishwa kwa Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma na kuimarisha mfumo wa uratibu na ufuatiliaji wa Mkakati kwa wadau wote.

Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji Awamu ya Kwanza (NACSAP I) ulikuwa na malengo 4 yafuatayo:

(i) Kutunga Sheria pana ya kukabiliana na rushwa;

(ii) Kubaini maeneo shawishi ya rushwa katika Serikali;

(iii) Kubaini hatua na mifumo ya kisheria na utawala ambayo itasaidia kudhibiti rushwa; na

(iv) Kujenga ubia kati ya Serikali na AZAKI zikihusisha Sekta Binafsi, Taasisi za Kitaaluma, Vyama vya Wafanyakazi na Taasisi za Kidini kuhusu mapambano dhidi ya rushwa.

Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa (NACSAP I) ulitoa maeneo sita ya kipaumbele katika utekelezaji wake ambayo ni:

**(i) Utawala wa Sheria**: Kusimamia sheria ili kuwajengea wananchi imani kuhusu Mahakama na Mawakala wake;

**(ii) Nidhamu ya Matumizi ya Fedha za Umma**: Kujenga nidhamu ya matumizi ya fedha za

umma kwa kuzuia ubadhirifu na kuongeza makusanyo ya fedha ili kuwezesha Serikali kutoa huduma bora kwa wananchi;

(iii) **Manunuzi ya Umma**: Kuhakikisha uzingatiaji wa taratibu za manunuzi ya umma na kuongeza uwazi katika usimamizi wa mchakato wa utoaji wa zabuni;

(iv) **Kutoa elimu kwa umma**: Kutoa elimu kwa umma kuhusu rushwa na madhara yake katika maendeleo ya uchumi;

(v) **Uwajibikaji**: Kujenga misingi ya uwajibikaji kwa Watumishi wa Umma; na

(vi) **Vyombo vya Habari**: Kutoa taarifa zenye kufichua rushwa bila woga au upendeleo kwa kutumia vyombo vya habari.

## 2.2 Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji Awamu ya Kwanza

### 2.2.1 Mafanikio

Utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji Awamu ya Kwanza umepata mafanikio makubwa yaliyotoa matokeo ya kuimarika utawala bora na uwajibikaji. Maboresho mengine katika Sekta ya Umma nayo yameimarisha utawala bora hasa katika nyanja za demokrasia na haki za binadamu na kujenga mifumo ya kitaasisi na kisheria. Katika kipindi cha utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Kwanza kati ya Mwaka 2001 hadi 2005

yalipatikana mafanikio yafuatayo:

i) Kuanzishwa kwa Ofisi za TAKUKURU hadi katika ngazi za Wilaya;
ii) Kuanzishwa kwa Taasisi mpya Simamizi za Masuala ya Utawala Bora na kupambana na rushwa. Taasisi hizo ni Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora na Kitengo cha Uratibu wa Utawala Bora - Ikulu;
iii) Kuanzishwa kwa Mamlaka ya Manunuzi ya Umma na Mamlaka ya Rufaa ya Manunuzi ya Umma chini ya Sheria ya Manunuzi ya Umma Na. 21 ya Mwaka 2001;
iv) Kuongezeka kwa uwazi na uwajibikaji katika utoaji wa huduma za umma;
v) Kuongezeka kwa uelewa wa umma kuhusu rushwa na madhara yake;
vi) Kubainisha maeneo yenye ushawishi wa rushwa.

Utafiti wa **Afro Barometer** uliofanywa na Taasisi ya Utafiti wa Jinsi ya Kupunguza Umaskini- REPOA (2005) ulionesha kuwa Serikali ilifanya vyema katika eneo la utawala bora na viashiria vya rushwa. Utafiti huo ulitathmini uelewa wa wananchi kuhusu dhana ya rushwa, jitihada za Serikali katika mapambano dhidi ya rushwa, hali ya rushwa kwa mtu mmoja mmoja na taasisi za Serikali, jinsi wananchi wanavyochukua hatua wanapodaiwa hongo na kiwango cha rushwa wakati wa mchakato wa uchaguzi. Kadhalika, walitathmini uwezo wa Serikali wa kusimamia Sheria dhidi ya Rushwa na makosa mengine ya jinai.

Taasisi ya Benki ya Dunia iliyotathmini mabadiliko ya utawala bora barani Afrika Mwaka (1996 – 2004) ilihusisha kudhibiti rushwa, ushirikishwaji, uwajibikaji na ufanisi katika utawala, uliiweka Tanzania miongoni mwa nchi zilizokuwa zinafanya vizuri katika nyanja hizo. Pia, Tanzania kupitia vigezo vya **Transparency International,** imeonesha kufanya vizuri katika **Corruption Perception Index** kwa kuongezeka kwa ubora kutoka alama **2.5** (2003) hadi **2.9** (2005).

### 2.2.2 Changamoto

Changamoto zinazohusisha utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji wa Awamu ya Kwanza zimeainishwa katika taarifa ya tathmini ya Programu ya Maendeleo ya Umoja wa Mataifa (UNDP) iliyofanyika chini ya Mradi wa kuimarisha na kujenga Uwezo wa Kukabiliana na Rushwa Tanzania ya Mwaka, 2004 ambazo ni:-

i) Ushirikishwaji mdogo au kutoshirikishwa kabisa kwa wadau muhimu kama vile Mamlaka za Serikali za Mitaa (TAMISEMI);

ii) Kutoshirikishwa kwa sekta binafsi katika utekelezaji wa Mkakati huu;

iii) Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa haukushirikisha AZAKI na pia ulishindwa kuainisha majukumu ya wadau katika utekelezaji wa Mkakati;

iv) Uhaba wa rasilimali watu na uwezo wa Taasisi

Simamizi kiutendaji uliathiri utekelezaji wa Mkakati;

v) Ukosefu wa Jukwaa la Kitaifa linalotoa nafasi ya mjadala wa wazi kuhusu rushwa;

vi) Wanasiasa kushiriki katika vitendo vya rushwa kwa kutoa zawadi kwa wapiga kura hasa nyakati za uchaguzi.

Kwa kuzingatia changamoto hizo, Serikali iliamua kuandaa na kutekeleza Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji wa Awamu ya Pili ili kuongoza mapambano dhidi ya rushwa nchini.

### 2.3 Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji Awamu ya Pili

Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji Awamu ya Pili (NACSAP II) ulizinduliwa Mwaka 2006 ili kukabiliana na changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa Mkakati wa Awamu ya Kwanza, kuendeleza mafanikio yaliyopatikana na kuufanya Mkakati huo kuwa shirikishi kwa madhumuni ya kupanua wigo wa mapambano dhidi ya rushwa nchini.

Mkakati huo ulitekelezwa kuanzia Mwaka 2006 hadi Mwaka 2011 ukiwa na madhumuni ya kurekebisha mapungufu ya Mkakati uliopita ya kutofunganisha jitihada zingine za maboresho katika Sekta ya Umma kama vile; Programu za Maboresho ya Utumishi wa Umma (PSRP), Udhibiti wa Fedha za Umma (PFMRP),

Sekta za Fedha (FSRP), Sekta ya Sheria (LSRP), Serikali za Mitaa (LGRP), Sekta ya Biashara (BEST) na Mkakati wa Taifa wa Kukuza na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA 2005 – 2010).

Kwa kutambua kuwa mapambano dhidi ya rushwa yamejengwa kutokana na Kanuni za Utawala Bora, hapana budi Mkakati wa Mapambano Dhidi ya Rushwa kuingizwa kwenye mfumo wa kawaida wa Utawala Bora wa kidemokrasia. Hivyo, Mkakati ulikusudia kusisitiza uwajibikaji na kujikita kwenye maboresho ya Sekta za Umma hususan katika Usimamizi wa Fedha za Umma (PFMRP) na Sekta ya Sheria (LSRP) ili kuzuia mianya ya upotevu wa fedha za umma na vitendo ya rushwa katika huduma zitolewazo na Taasisi za Umma.

Moja ya madhumuni ya Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji Awamu ya Pili yalikuwa ni kutunga Sheria ambayo itaimarisha mapambano dhidi ya rushwa, ikilenga maeneo yenye ushawishi wa rushwa na kushauri njia bora zitakazotokomeza vitendo vya rushwa Serikalini. Mkakati wa Awamu ya Pili, uliangalia hatua bora za kisheria na kiutawala katika kushughulikia vitendo vya rushwa na kuweka programu zitakazosaidia uungwaji mkono wa jamii hususan Asasi za Kiraia, Sekta Binafsi, Taasisi za Dini na Wanazuoni katika mapambano dhidi ya rushwa.

Njia iliyotumika kutekeleza Mkakati huu ni kushirikisha wadau wote wakiwemo Sekta Binafsi, Sekta ya Umma na

Asasi za Kiraia ili kuelewa majukumu yao na kuhusika kikamilifu katika mchakato wa kupunguza rushwa nchini. Mkakati wa Awamu ya Pili ulitoa fursa kwa wadau kutafsiri Sera za Serikali za Mapambano Dhidi ya Rushwa na kuziweka katika programu zinazotekelezeka.

### 2.3.1 Malengo ya Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji Awamu ya Pili

Malengo ya Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Pili yalikuwa ni:

(i) Kuongeza uelewa kwa umma kuhusu mapambano dhidi ya rushwa;
(ii) Kupanua wigo wa mapambano dhidi ya rushwa;
(iii) Kuboresha na kuimarisha huduma za Umma;
(iv) Kuimarisha Taasisi Simamizi za Masuala ya Utawala Bora;
(v) Kuhimiza Uwazi, Uwajibikaji na Uadlifu katika utekelezaji wa shughuli za Umma; na
(vi) Kuwezesha Asasi Zisizokuwa za Kiserikali, Sekta Binafsi, Asasi za Kiraia na Vyombo vya Habari kushiriki kikamilifu katika mapambano dhidi ya rushwa.

Mkakati wa Awamu ya Pili ulikuwa chombo kilichohimiza uwazi, uwajibikaji na uadilifu katika kutekeleza majukumu ya umma. Ulitoa fursa ya kutafsiri Sera za Serikali kuhusu mapambano dhidi ya rushwa kwa vitendo.

Katika Mkakati huo, kila Wizara, Idara inayojitegemea, Wakala wa Serikali na Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zilitakiwa kuandaa Mpango Kazi wake. Ili kuhakikisha utekelezaji wenye ufanisi, Serikali ilianzisha Kitengo cha Uratibu wa Utawala Bora, Ofisi ya Rais – Ikulu na kuweka mfumo wa ufuatiliaji utakaozalisha taarifa za utekelezaji za robo mwaka kutoka Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala wa Serikali, Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**2.3.2 Mfumo wa Sheria na Kitaasisi**

Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji Awamu ya Pili ulilenga kuimarisha Utawala Bora kisheria na kitaasisi kama ifuatavyo:

i) **Sheria ya Utumishi wa Umma Na.8 ya Mwaka 2002 na Kanuni zake za Mwaka 2003**

Sheria hii inalenga kuimarisha kiwango cha ubora wa huduma, menejimenti ya rasilimali watu na vyombo vya mamlaka ya nidhamu kama vile Tume ya Utumishi wa Umma.

ii) **Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali**

Sheria ya Ukaguzi ya Umma Na.11 ya Mwaka 2008 inaimarisha majukumu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali juu ya matumizi ya fedha za Umma kama Msimamizi Mkuu wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi. Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za

Serikali ni huru kama ilivyoelezwa kwenye Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

iii) **Mamlaka ya Mapato Tanzania**
Mamlaka ya Mapato Tanzania imeundwa chini ya Sheria ya Mapato Na. 11 ya Mwaka 1995 ili kuimarisha na kuboresha ukusanyaji wa mapato Serikalini. Hatua kadhaa zimechukuliwa za kupambana na kupunguza uwezekano wa kufanyika vitendo vya rushwa ikiwa ni pamoja na kufungamanisha mifumo ya ukaguzi katika vitengo vya kodi (*Income Tax, Import, Export and Excise Duty*) na Idara ya Kodi ya Ongezeko la Thamani ili kuongeza uwazi na uwajibikaji.

iv) **Baraza la Maadili**
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa Awamu ya Nne aliteua Wajumbe wa Baraza la Maadili Mwaka 2009 chini ya Kifungu cha 26 (1) cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Na.13 ya Mwaka 1995 ili kutekeleza matakwa ya Sheria.

v) **Wakala ya Serikali Mtandao**
Wakala ya Serikali Mtandao ni matokeo ya taarifa ya Tume ya Rais ya Kero ya Rushwa iliyoratibiwa na Jaji Warioba Mwaka 1996. Juhudi zimekuwa zikifanyika kuhakikisha

Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala wa Serikali, Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa wanashirikishwa kikamilifu katika kutoa huduma kwa njia ya mtandao "*e-Government initiatives*". Vilevile, mwaka 2012 Serikali ilianzisha Wakala ya Serikali Mtandao ili kuziwezesha Taasisi zingine za Umma kuweka na kuanza kutumia mifumo ya TEHAMA inayohusiana na huduma wanazozitoa, ikiwa ni pamoja na kampeni ya utumaji wa ujumbe mfupi wa maneno wa vitendo vya rushwa na kuanzishwa kwa Tovuti Kuu ya Serikali.

vi) **Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Manunuzi ya Umma**

Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Manunuzi ya Umma iliundwa chini ya Sheria ya Ununuzi Na. 21 ya Mwaka 2004 kwa lengo la kusimamia taratibu za ununuzi wa mali za Umma na kuimarisha majukumu ya ununuzi. Kitengo cha Manunuzi ya Mali za Umma kilianzishwa katika Wizara ya Fedha chini ya Sheria ya Manunuzi ya Umma Na. 7 ya Mwaka 2011 ambacho kina jukumu la kuzingatia taratibu za manunuzi na kuzijengea uwezo Taasisi za Umma.

### 2.3.3 Muundo wa Utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji Awamu ya Pili

#### 2.3.3.1 Kamati ya Taifa ya Uendeshaji

Kamati ya Taifa ya Uendeshaji iliundwa katika ngazi ya Taifa ili kutoa miongozo ya kisera na kimkakati katika utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa. Wajumbe wa Kamati walitoka Kitengo cha Uratibu wa Utawala Bora, Ofisi ya Rais – Ikulu, TAKUKURU, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Ofisi ya Waziri Mkuu, Programu za Maboresho ya Matumizi ya Fedha za Umma, Sekta ya Umma, Serikali za Mitaa, Asasi za Kiraia, Vyombo vya Habari, Sekta Binafsi, Jumuiya ya Tawala za Serikali za Mitaa *(ALAT)*, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA), Programu ya Maendeleo ya Umoja wa Mataifa na wawakilishi wa Wabia wa Maendeleo.

#### 2.3.3.2 Jukwaa la Kitaifa la Mapambano Dhidi ya Rushwa

Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa, Awamu ya Pili ulianzisha Jukwaa la Kitaifa la Mapambano Dhidi ya Rushwa lililokutana mara moja kwa mwaka kwa lengo la wadau kujadili na kubadilishana uzoefu katika utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Pili.

#### 2.3.3.3 Kamati za Kudhibiti Uadilifu

Kamati za Kudhibiti Uadilifu ziliundwa katika kila

Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuratibu utekelezaji wa Mkakati wa Awamu ya Pili.

### 2.3.4 Jitihada zingine zilizotekelezwa sanjari na Mkakati wa Taifa dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji Awamu ya Pili

#### 2.3.4.1 Mpango wa Kujitathmini wa Nchi za Kiafrika

Mwaka 2004 Tanzania ilijiunga kwa hiari na Mpango wa Kujitathmini wa Nchi za Kiafrika ambapo Mwaka 2012 ilitathminiwa na taarifa yake kuchapishwa na kuwasilishwa kwa Wakuu wa Nchi wa Umoja wa Afrika Januari, 2013. Taarifa ilibainisha juhudi zinazofanywa na nchi katika kuimarisha utawala bora na mapambano dhidi ya rushwa ambapo juhudi hizi zinaungwa mkono na Umoja wa Afrika hususan Sera ya Tanzania ya Kutovumilia Vitendo vya Rushwa.

#### 2.3.4.2 Mpango wa Kuendesha Shughuli za Serikali kwa Uwazi

Mpango wa Kuendesha Shughuli za Serikali kwa Uwazi ni Mpango wa Kimataifa unaolenga kukuza Uwazi, Ushirikishwaji wa Wananchi, Mapambano Dhidi ya Rushwa na kuhimiza matumizi ya Teknolojia ili kuboresha Utawala Bora. Tanzania iliamua kujiunga na Mpango wa Kuendesha Shughuli za Serikali kwa Uwazi ili kuunga mkono juhudi nyingine zinazofanywa na Serikali katika kukuza na kuimarisha utawala bora katika Sekta zote.

Kanuni za Mpango wa Kuendesha Shughuli za Serikali kwa Uwazi zinashabihiana na Mpango wa Utawala Bora ulioundwa Mwaka 1999 katika kuimarisha Utawala Bora nchini. Hivyo, Mpango wa Kuendesha Shughuli za Serikali kwa Uwazi ni jitihada za ziada katika kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Mapambano Dhidi ya Rushwa ili kuimarisha uwajibikaji, uwazi na uadilifu nchini.

**2.3.4.3 Mpango wa Msaada wa Kibajeti**

Wabia wa Maendeleo wamekuwa wakichangia Bajeti ya Taifa ya Tanzania kwa kuzingatia vigezo vya utekelezaji vya Utawala Bora vilivyokubalika na Serikali. Hivyo, Wabia wa Maendeleo hufanya tathmini ya mara kwa mara ya utekelezaji wa vigezo hivyo hususan uwazi katika bajeti, haki ya kupata taarifa, ubora wa mahusiano na majadiliano kati ya Serikali na wadau wa ndani na Uwajibikaji wa Serikali kwa Bunge.

Taarifa hizo zinaonesha kuwa Tanzania imekuwa ikiendelea kuboresha huduma zake katika vipindi vyote vya tathmini kuanzia Mwaka 2002 hadi 2011.

### 2.3.5 Mafanikio na Changamoto za Utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Pili

#### 2.3.5.1 Mafanikio

Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji Awamu ya Pili ulipata mafanikio yafuatayo:

i) Kutungwa kwa Sheria pana ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Na. 11 ya Mwaka 2007 ambayo imeongeza makosa ya rushwa hadi 24 ikilinganishwa na makosa manne (4) yaliyokuwa kwenye Sheria ya Kuzuia Rushwa Na. 16 ya Mwaka 1971 iliyofutwa;

ii) Kuongeza uelewa kwa umma kuhusu makosa ya rushwa pamoja na masuala ya uwazi na uwajibikaji;

iii) Kuimarisha uwezo wa TAKUKURU hususan kwa kuanzisha Ofisi katika Wilaya zote nchini na hivyo kuwezesha kuzuia na kupambana na rushwa katika ngazi ya chini;

iv) Kufanya Utafiti wa Msingi Mwaka 2009 ili kutathmini hali ya rushwa na utawala bora nchini. Rushwa ilionekana inapungua taratibu na utawala bora ukiongezeka;

v) Serikali kuridhia Itifaki za Kikanda na Kimataifa zikiwemo za Nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika, Umoja wa Afrika na Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mapambano dhidi ya

Rushwa;

vi) Kuanzishwa kwa Kamati za Kudhibiti Uadilifu katika Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ambazo zilipewa jukumu la kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Mkakati katika sehemu zao za kazi; na

vii) Ushirikishwaji wa Asasi zisizo za Kiserikali katika utekelezaji wa Mkakati.

**2.3.5.2 Changamoto**

Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji Awamu ya Pili ulikuwa na changamoto zifuatazo:

(i) Ukosefu wa muendelezo, utekelezaji wa majukumu na kudumu kwa Kamati za Kudhibiti Uadilifu uliosababishwa na:

- Kushindwa kuendesha mafunzo kwa wajumbe wa Kamati za Kudhibiti Uadilifu;
- Kushindwa kuwabakiza wajumbe wa Kamati za Kudhibiti Uadilifu kuendelea kutekeleza majukumu yao kwenye Taasisi, Idara za Serikali, Wizara, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa; na
- Baadhi ya Wajumbe wa Kamati za Kudhibiti Uadilifu kutofikia vigezo vya uadilifu vinavyotakiwa;

(ii) Kutozingatiwa kwa Sheria, Kanuni na Taratibu unaotokana na udhaifu katika utoaji wa adhabu, usimamizi hafifu na ukosefu wa motisha;

(iii) Uhaba wa fedha;

(iv) Kutokuwepo kwa utashi thabiti kwa Wadau wa kutekeleza Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa;

(v) Kutokuwepo kwa Mfumo rasmi wa Uratibu wa Mkakati katika ngazi ya Mkoa na Wilaya;

(vi) Ugumu wa kupata ushahidi wa kesi za rushwa hususan kesi zinazohitaji kufanyika upelelezi nje ya Nchi;

(vii) Kukosekana kwa Mwongozo wa kuhusisha Viongozi wa Dini katika kusimamia maendeleo na utekelezaji wa miradi katika Serikali za Mitaa ili kupambana na rushwa;

(viii) Kutokuwepo kwa utaratibu toshelevu wa kubadilishana taarifa na AZAKI zinazosimamia mapambano dhidi ya rushwa;

(ix) Udhaifu wa Taasisi Simamizi za Masuala ya Utawala Bora katika utekelezaji wa Mkakati wa Awamu ya Pili; na

(x) Mifumo hafifu ya Ufuatiliaji na Tathmini ya utekelezaji wa Mkakati.

Ukuzaji wa utawala bora na kupunguza vitendo vya rushwa ni jambo muhimu kwa ukuaji wa uchumi na maendeleo ya Nchi, haki na usawa, utawala wa sheria, amani na utulivu kwa ujumla. Hii inahitaji kuunganisha nguvu za pamoja ambazo zitawezesha Serikali na Wadau kubuni njia ambazo zitatumika katika kuzuia na kupambana na rushwa.

Hivyo, Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji Awamu ya Tatu umeandaliwa kwa kuzingatia mahitaji ya sasa na kutanzua changamoto zilizojitokeza. Madhumuni ya Mkakati wa Awamu ya Tatu yamejikita katika mbinu za kuzuia na kupambana na rushwa na kuweka kipaumbele katika kuimarisha Ufuatiliaji na Tathmini, Kuimarisha utawala wa Sheria, Kubuni mbinu mpya za kuzuia na kupambana na rushwa, Kukuza Maadili, Ushirikishwaji wa Wadau, Utekelezaji wa adhabu, usimamizi na kutoa motisha katika mapambano dhidi ya rushwa.

# SURA YA TATU
# MKAKATI WA TAIFA DHIDI YA RUSHWA NA MPANGO WA UTEKELEZAJI AWAMU YA TATU

## 3.0 Utangulizi

Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji Awamu ya Tatu ni mwendelezo wa jitihada mtambuka katika kuendeleza mapambano dhidi ya rushwa nchini. Mipango na hatua kadhaa zimechukuliwa kuendeleza mafanikio yaliyopatikana na kukabiliana na changamoto za jitihada zilizopita zilizolenga kujenga Jamii na Taasisi ikiwa ni pamoja na mifumo madhubuti ya ufuatiliaji na tathmini ambayo itaendeleza Sera ya Kutovumilia Rushwa. Utekelezaji wa Mkakati wa Awamu ya Tatu utashirikisha wadau muhimu zikiwemo AZAKI, Sekta Binafsi, Vyombo vya Habari, Wataalamu, Vyama vya Siasa, Vyama vya Wafanyakazi, Taasisi za Dini, Sekta ya Umma na Wabia wa Maendeleo.

## 3.1 Lengo Kuu la Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji Awamu ya Tatu

Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji Awamu ya Tatu umeandaliwa kwa kuzingatia vipaumbele vya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2017/18 – 2021/22), Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2015 na Hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli

wakati akizindua Bunge la 11 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 20 Novemba 2015 mjini Dodoma. Mkakati utatumia njia madhubuti katika mapambano dhidi ya rushwa na kuboresha utawala bora kwa kuwa na uongozi imara. Mkazo umewekwa katika kutekeleza Sera ya Kutovumilia Rushwa, kuboresha utawala, kubadili mtazamo na hivyo kuwa watu wa vitendo, kutoa maamuzi kwa wakati na Mashirika ya Umma kujiendesha kibiashara na kwa tija.

Aidha, utekelezaji wa Mkakati huu utajikita katika kushughulikia sekta za kimkakati katika kuzuia na kupambana na rushwa katika manunuzi ya umma, ukusanyaji wa mapato, uvunaji na matumizi ya maliasili, madini, nishati, mafuta na gesi, utawala, vyombo vya utoaji wa haki na shughuli za Vyama vya Siasa. Mkakati pia utakuwa na malengo na shughuli za kuzuia na kupambana na rushwa katika maeneo ya utoaji huduma, ambayo yanashusha uhalali na Mamlaka ya Serikali. Hivyo, lengo kuu la Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji Awamu ya Tatu ni **Kupunguza Rushwa nchini kwa kutumia mbinu za kuzuia na kupambana na rushwa kwa kuweka mkazo katika sekta zenye ushawishi wa rushwa**.

Malengo mahususi ya Mkakati ni:

(i) Kuimarisha ufanisi, uwazi na uwajibikaji wa utoaji wa huduma katika Sekta ya Umma na Binafsi;

(ii) Kuwa na ufanisi katika utekelezaji wa mikakati ya mapambano dhidi ya rushwa;

(iii) Kuzijengea uwezo Taasisi Simamizi za Masuala ya Utawala Bora; na

(iv) Kuwa na Uongozi madhubuti wa kisiasa unaoshiriki kwa dhati katika mapambano dhidi ya rushwa.

Malengo haya yatafikiwa kupitia utekelezaji wa mikakati ifuatayo:

**(i) Kuweka kipaumbele kwenye sekta na maeneo yenye ushawishi wa rushwa**

Hatua za kimkakati katika mapambano dhidi ya rushwa zitaelekezwa katika sekta yenye ushawishi wa rushwa ili kupata thamani halisi ya kitu au huduma, kuboresha utoaji huduma na hivyo kurejesha imani ya umma kwa Serikali. Maeneo ya kipaumbele ni pamoja na manunuzi ya umma, ukusanyaji wa mapato, utawala wa sheria, Polisi, Afya, Elimu na matumizi ya maliasili. Hatua za kukabiliana na rushwa katika sekta hizi ni pamoja na kuainisha maeneo yenye ushawishi wa rushwa, kubaini vyanzo vya rushwa/vitendo visivyokuwa vya kimaadili na kuchukua hatua stahiki, kufanya upembuzi wa vihatarishi vya rushwa, kufanya upembuzi wa uzingatiaji wa sheria na taratibu za kazi, kuendesha programu za uelimishaji umma na kampeni za mapambano dhidi ya rushwa.

(ii) **Kuimarisha utekelezaji wa sheria, usimamizi na utoaji wa motisha katika mapambano dhidi ya rushwa**

Kumekuwepo na usimamizi wa sheria, kanuni na taratibu usioridhisha ambao matokeo yake ni kuwepo kwa adhabu ndogo, usimamizi dhaifu na kutokuwepo kwa mfumo wa utoaji motisha katika kuzuia na kupambana na rushwa. Hivyo, sheria, kanuni na taratibu za mapambano dhidi ya rushwa zitafanyiwa mapitio, zitahuishwa, kutungwa, kusimamiwa na kutekelezwa ipasavyo.

(iii) **Kuimarisha na kuwezesha umma kushiriki katika kudai haki na uwajibikaji wa Serikali**

Ushiriki wa wananchi katika kudai haki zao na uwajibikaji wa Serikali ni mdogo. Hivyo, mazingira wezeshi yatawekwa ili kuhakikisha ushiriki kamilifu wa wananchi katika mapambano dhidi ya rushwa, kudai haki zao za msingi na uwajibikaji kupitia programu za elimu kwa umma.

(iv) **Kuimarisha elimu ya maadili na mapambano dhidi ya rushwa kupitia Mkakati wa Habari, Elimu na Mawasiliano**

Ushiriki kamilifu wa AZAKI, Taasisi za Dini na Sekta Binafsi ni muhimu katika mapambano

dhidi ya rushwa. Jitihada kubwa za kuelimisha AZAKI, Taasisi za Dini na Sekta Binafsi zinahitajika ili kuimarisha ushiriki wao. Kwa muktadha huu, elimu kwa umma kuhusu utawala bora na sheria ni nyenzo muhimu katika mapambano dhidi ya rushwa. Hivyo, Mkakati wa Habari, Elimu na Mawasiliano utaandaliwa na kutekelezwa ipasavyo.

**(v) Kuimarisha ubia na ushirikiano miongoni mwa Serikali, AZAKI, Bunge, Mahakama, Vyama vya Siasa, Vyombo vya Habari, Sekta Binafsi na Wabia wa Maendeleo**

Mapambano dhidi ya rushwa hayahitaji tu nguvu ya pamoja bali pia ushirikiano wa wadau mbalimbali. Hivyo, ushirikiano baina ya wadau utaimarishwa ili kuendeleza uadilifu.

**(vi) Kuimarisha na kuboresha mifumo ya utawala wa vyombo vya utoaji wa haki**

Mpango wa kutenganisha shughuli za upelelezi na mashtaka umewezesha kupunguza urasimu katika uendeshaji wa mashtaka. Aidha, Ofisi ya Mtendaji Mkuu wa Mahakama Tanzania imeanzishwa ili kutekeleza masuala ya utawala katika shughuli za Mahakama. Kuweka mazingira wezeshi ikiwemo elimu na vitendea kazi kwa vyombo vyote vinavyosimamia utoaji haki (TAKUKURU, Polisi, Magereza na Ofisi ya

Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kuendeleza weledi na utoaji haki sawa kwa wote.

(vii) **Kuimarisha na kujenga uwezo wa Taasisi Simamizi za Masuala ya Utawala Bora, Kamati za Kudhibiti Uadilifu na Kamati za Uratibu wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa za Wizara, Idara za Serikali Zinazojitegemea, Wakala wa Serikali, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Bunge, Mahakama na Asasi zisizokuwa za Kiserikali**

Taasisi Simamizi za Masuala ya Utawala Bora zinakabiliwa na changamoto nyingi ambazo zinaathiri utendaji wao. Mifumo madhubuti na kujenga uwezo kwa maana ya kutoa elimu na vitendea kazi ili kuendeleza weledi, uadilifu na utoaji haki.

(viii) **Kuweka mkazo wa matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma**

Uzoefu umeonyesha kuwa matumizi ya TEHAMA yameleta ufanisi na kupunguza vitendo vya rushwa katika utoaji wa huduma hasa baada ya mfumo wa malipo kwa njia ya elekroniki kuanza kutumika (Manunuzi, Makusanyo ya Mapato na Kodi). Hivyo, Mkakati utasisitiza matumizi mapana ya mifumo ya TEHAMA ili kuhakikisha ufanisi na

uwajibikaji katika kutoa huduma nchini.

**(ix) Kukuza uwazi na uwajibikaji katika utekelezaji wa shughuli za Umma na Binafsi**

Kanuni na taratibu katika kuendesha shughuli za Ofisi au shughuli za biashara kwa manufaa ya umma zitatekelezwa ili kuhakikisha uwepo wa uwazi na uwajibikaji.

**(x) Kuingiza elimu ya maadili na masuala ya rushwa kwenye mitaala na mifumo ya elimu kwa Shule za Msingi, Sekondari, Vyuo vya Elimu ya Juu wakiwemo vijana walio nje ya mfumo rasmi wa elimu**

Mfumo wa elimu, hasa mitaala ya elimu ya maadili na rushwa ni nyenzo muhimu katika kujenga tabia ya kitaifa na utamaduni wa mapambano dhidi ya rushwa. Hatua muhimu katika mapambano dhidi ya rushwa zitachukuliwa kwa kuingiza elimu ya maadili na masuala ya rushwa kwenye mitaala na mifumo ya elimu kwa Shule za Msingi, Sekondari, Vyuo vya Elimu ya Juu wakiwemo vijana walio nje ya mfumo rasmi wa elimu ili kujenga weledi na uadilifu katika jamii.

(xi) **Kuimarisha uratibu wa ufuatiliaji na tathmini katika utekelezaji wa Mkakati nchini**

Ili kuhakikisha utekelezaji madhubuti wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa, mfumo mzuri wa ufuatiliaji na tathmini na muongozo wa utekelezaji wa Mkakati utaandaliwa na kutekelezwa ipasavyo. Mfumo wa ufuatiliaji na tathmini utajengwa ili kuwa na kanzidata yenye malengo na viashiria vya utekelezaji.

## 3.2 Nyenzo za Utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji Awamu ya Tatu

Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji Awamu ya Tatu utasaidiwa na nyenzo za utekelezaji zifuatazo:

### 3.2.1 Mipango Kazi

Taasisi za Umma zitatakiwa kuandaa na kutekeleza mipango kazi ya Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Tatu itakayozingatia masuala muhimu ya utawala yakiwemo rushwa na ukiukwaji wa maadili ya utumishi wa umma. Maudhui ya mipango kazi yatazingatia Mwongozo wa Utekelezaji wa Mkakati ulioidhinishwa. Sekta Binafsi na Taasisi Zisizokuwa za Kiserikali nao wanategemewa kuandaa na kutekeleza mpango kazi husika katika maeneo yao ya kazi.

### 3.2.2 Kamati za Kudhibiti Uadilifu

Kutakuwa na Kamati za Kudhibiti Uadilifu kwa kila Taasisi ya Umma, Sekta Binafsi na Taasisi Zisizokuwa za Kiserikali ambazo wajumbe wake watateuliwa na Wakuu wa Taasisi husika. Idara za Utumishi na Rasilimaliwatu zitakuwa sekretarieti kwa kamati hizo. Wajumbe wanapaswa kuwa na sifa ya kuwa Maafisa Waandamizi wenye haiba ya uadilifu. Mkuu wa Taasisi atateua wajumbe pamoja na Mwenyekiti na kuwasilisha majina yao kwa Katibu Mkuu Kiongozi kwa taarifa na kumbukumbu. Kamati zitachukua jukumu la kusimamia utekelezaji wa Mkakati.

### 3.2.3 Jukwaa la Kitaifa la Mapambano Dhidi ya Rushwa

Jukwaa hili ni mahali ambapo wadau mbalimbali kutoka Serikalini, Asasi zisizokuwa za Kiserikali hukutana, kujadiliana na kutathmini utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa. Jukwaa litafanyika mara moja kwa mwaka na litatumika pia kujenga mahusiano baina ya wadau katika Sekta ya Umma na Asasi Zisizokuwa za Serikali.

Jukwaa hilo litatumika kama fursa kwa wadau kubadilishana mawazo na uzoefu wa taarifa za utekelezaji wa Mkakati na kupendekeza mipango na mikakati ya baadaye. Aidha, jukwaa hilo pia litachangia katika kujenga uelewa kwa Umma kuhusu rushwa na madhara yake. Ujumbe unaopatikana kutoka kwenye Jukwaa utawezesha wananchi kujengewa uwezo wa kutambua

haki, wajibu na kushiriki kikamilifu katika mapambano dhidi ya rushwa badala kushabikia kauli mbiu za mapambano dhidi ya rushwa.

### 3.2.4 Kamati ya Taifa ya Uendeshaji

Kutakuwa na Kamati ya Taifa ya Uendeshaji itakayosimamia uratibu na utekelezaji wa Mkakati na Mapambano Dhidi ya Rushwa Awamu ya Tatu. Wajumbe wa Kamati hiyo watateuliwa na Katibu Mkuu Kiongozi na watatoka katika Taasisi Simamizi za Masuala ya Utawala Bora, Programu za Maboresho mtambuka na Taasisi Zisizokuwa za Kiserikali wakiwemo Taasisi za Kiraia, Vyombo vya Habari, Sekta Binafsi na Taasisi za Dini. Wajumbe wanatakiwa kuwa Maafisa Waandamizi waadilifu.

### 3.2.5 Kamati ya Taifa ya Kitaalam ya Ushauri

Kamati ya Taifa ya Kitaalam ya Ushauri itaundwa na Taasisi Simamizi za Masuala ya Utawala Bora chini ya Uenyekiti wa Katibu Mkuu Kiongozi. Kamati hii itakuwa na jukumu la kutoa ushauri na kusimamia utekelezaji wa Mkakati wakati wote.

### 3.2.6 Uratibu wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji Awamu ya Tatu

Ofisi ya Katibu Mkuu Kiongozi kupitia Kitengo cha Uratibu wa Utawala Bora itaratibu utekelezaji wa Mkakati ngazi ya Taifa. Taasisi za Umma zitapaswa kuandaa mipango kazi pamoja na taarifa za utekelezaji kila robo

mwaka na kuwasilisha katika Kitengo hicho kwa wakati.

### 3.2.7 Ubia na Ushirikiano katika Mapambano Dhidi ya Rushwa na Taasisi za Kitaifa, Kikanda na Kimataifa

Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji Awamu ya Tatu utazingatia misingi na masharti ya taasisi na itifaki za Kitaifa, Kikanda na Kimataifa kwa lengo la kujenga mtangamano wa ushirikiano miongoni mwa taasisi husika. Itifaki hizo ni pamoja na Mkataba wa Umoja wa Mataifa, Itifaki ya Umoja wa Afrika na Itifaki ya Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika katika mapambano dhidi ya rushwa. Aidha, Taasisi nyingine ni Wakala wa Kimataifa wa Mapambano Dhidi ya Rushwa, Nchi za Afrika Mwanachama wa Jumuiya ya Madola na Mtandao wa Wabunge wa Afrika wanaopinga rushwa.

### 3.2.8 Programu za Kujenga Uwezo kwa Taasisi Zisizokuwa za Kiserikali

Kutaandaliwa programu za kujenga uwezo wa Taasisi Zisizokuwa za Kiserikali kuhusu kuzuia na kupambana na rushwa hususan mafunzo, vitendea kazi na rasilimali fedha kwa lengo la kuwapa uwezo zaidi.

### 3.2.9 Mikataba ya Huduma kwa Wateja

Taasisi za Umma zitapaswa kuandaa na kuhuisha mikataba yao ya huduma kwa wateja ili kuimarisha uwazi na uwajibikaji kwa lengo la kuboresha utoaji huduma kwa umma.

### 3.2.10 Mfumo wa Kushughulikia Malalamiko

Mfumo wa kushughulikia malalamiko utaimarishwa na kutangazwa kwa wadau katika Taasisi za Umma kama chanzo cha kupokea taarifa za rushwa, kero na utendaji usioridhisha wa Serikali kutoka kwa watoa taarifa na wananchi kwa ujumla. Hivyo, Taasisi zinaelekezwa kuwa na mfumo wa kushughulikia malalamiko ili kukidhi matakwa hayo.

### 3.2.11 Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini

Mfumo madhubuti wa ufuatiliaji na tathmini ni nyenzo muhimu katika utekelezaji wa Mkakati. Hivyo, Taasisi za Umma na Asasi Zisizo za Kiserikali zitapaswa kuandaa mfumo wa ufuatiliaji na tathmini utakaozingatia muundo na mfumo wa Mpango wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Kitaifa. Mfumo huu utatumika katika kupima mafanikio ya utekelezaji wa Mkakati.

## 3.3 Vigezo Muhimu vya Kufanikisha Utekelezaji wa Mkakati

Kufanikiwa kwa utekelezaji wa Mkakati wa Awamu ya Tatu kunategemea sana wananchi watakavyoshiriki na kumiliki mchakato wa mapambano dhidi ya rushwa nchini. Mambo yanayoweza kufanikisha utekelezaji wa Mkakati ni pamoja na kuwepo kwa uongozi wa kimageuzi, sera bora, malengo yanayopimika, kampeni kwa umma, kuwepo kwa taarifa sahihi, ubora wa elimu ya mawasiliano kwa umma, kutenganisha shughuli za siasa na utawala, mifumo imara ya sheria na utoaji haki

na taasisi imara za usimamizi wa mapambano dhidi ya rushwa ngazi ya Kitaifa. Mambo mengine muhimu ni uhuru wa Vyombo vya Habari, uhuru wa vyombo vya utoaji wa haki, rasilimali za kutosha pamoja na kuwa na jamii inayokwenda na wakati.

### 3.3.1 Uongozi wa Kimageuzi

Uongozi wa kimageuzi ni mhimili mkubwa katika kufanikisha utekelezaji wa Mkakati wa Awamu ya Tatu. Hii inamaanisha kuwa na uongozi wenye nia ya dhati ya kukuza na kuendeleza utawala bora, uwepo wa utashi wa kisiasa, kuwa na dira inayoeleweka, uaminifu na uadilifu, ufanisi, kukubalika na kuheshimiwa na wananchi. Aina hii ya uongozi inahitajika katika Taasisi za Umma na Sekta Binafsi, Asasi Zisizokuwa za Kiserikali na Mashirika ya Dini. Uongozi huu wenye sifa tajwa ni dhahiri utaweza kuongeza ari na kushawishi wananchi kushiriki kikamilifu katika mapambano dhidi ya rushwa.

### 3.3.2 Sera Bora na Malengo yanayopimika

Sera bora na malengo yanayopimika yataandaliwa katika kutekeleza Mkakati. Kimsingi malengo yanayowekwa lazima yawe muhimu, yenye uwiano na uhalisia kulingana na mazingira ili yaweze kutatua changamoto za utekelezaji wa Mkakati katika maeneo ya Taasisi husika.

### 3.3.3 Habari, Elimu na Mawasiliano

Kufikiwa kwa malengo ya Mkakati wa Awamu ya Tatu kutategemea sana uwepo na upatikanaji wa habari, taarifa

na utoaji wa elimu kuhusu utawala bora na maadili katika ngazi mbalimbali katika sekta ya Umma na Binafsi katika jamii. Inatarajiwa kwamba, mipango kazi ya Taasisi za Umma itajumuisha suala la kuelimisha umma kuhusu maadili na Sera ya Kutovumilia Rushwa. Hivyo, Mkakati utahakikisha taasisi husika zinatoa elimu ya mapambano dhidi ya rushwa wakati wote ili kuwaongezea wananchi elimu ya uraia. Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa unachukulia kuwa programu za uelimishaji umma kama sehemu ya mkakati wa mawasiliano ambao ni nyenzo muhimu ya kuleta mafanikio katika utetekelezaji wa Mkakati. Kwa mantiki hii, Mkakati wa Habari, Elimu na Mawasiliano kama nyenzo muhimu ya utekelezaji wa Mkakati, utaandaliwa na kutekelezwa kikamilifu kwa lengo la kufanikisha utekelezaji wa Mkakati.

### 3.3.4 Kutenganisha Siasa na Shughuli za Utawala

Kutambua uwepo wa mipaka ya majukumu kati ya uongozi wa kisiasa, watendaji wa Serikali na Wafanyabiashara ni muhimu sana katika kutekeleza Mkakati. Wanasiasa pamoja na Vyama vya Siasa wanashauriwa kuwa mstari wa mbele katika kusimamia uhamasishaji wa masuala ya utawala bora ikiwemo kuzuia na kupambana na rushwa.

Hivyo, vyombo vya uendeshaji vya Serikali vinategemewa pia kutekeleza majukumu yake kwa dhati kwa kuzingatia taratibu zilizopo bila upendeleo, kwa weledi na zaidi ya yote, kwa kuzingatia maadili ya utumishi wa Umma, hususan wanaposhughulikia masuala yanayohusu Viongozi wa Kisiasa.

### 3.3.5 Mfumo Madhubuti wa Utoaji wa Haki na Uhuru wa Mahakama

Mkakati wa Awamu ya Tatu unatambua umuhimu wa kuwepo mfumo madhubuti wa utoaji haki usiojihusisha na vitendo vya rushwa. Mifumo huru ya utoaji haki itaharakisha utoaji haki, ambalo ni jambo muhimu katika kuujengea umma imani katika mifumo ya utawala. Hivyo, mifumo hiyo madhubuti inatarajiwa kuwezesha kuwepo kwa sheria zinazokidhi misingi ya utawala bora na mapambano dhidi ya rushwa.

### 3.3.6 Upatikanaji wa Rasilimali za Kutosha

Utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Kwanza na ya Pili, ulikabiliwa na changamato kubwa ya upatikanaji wa fedha na rasilimali zingine ikiwemo wataalamu wenye ujuzi. Katika kukabiliana na hilo Mkakati wa Awamu ya Tatu utahakikisha kwamba unatafuta fedha za kutosha, watumishi wenye weledi, matumizi ya teknolojia ambazo zitatolewa na Serikali, Sekta Binafsi na Wabia wa Maendeleo.

# SURA YA NNE

# MPANGILIO WA KITAASISI NA MAJUKUMU

## 4.0 Utangulizi

Mapambano dhidi ya rushwa yanahitaji ushiriki na ushirikishwaji thabiti wa wadau wote kutoka Sekta ya Umma na Asasi Zisizokuwa za Serikali chini ya uongozi wa Katibu Mkuu Kiongozi ambaye ni Msimamizi Mkuu wa utekelezaji wa Mkakati wa Awamu ya Tatu. Wadau wote wanapaswa kuweka kipaumbele katika jitihada za mapambano dhidi ya rushwa na wanaaswa kuandaa mazingira wezeshi ya utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji Awamu ya Tatu. Inatarajiwa kuwa kila mdau atakuwa mstari wa mbele katika kutambua, kuweka kipaumbele na kutekeleza hatua mbalimbali za kuzuia na kupambana na rushwa na vitendo vingine visivyo vya kimaadili. Hivyo, mapambano dhidi ya rushwa yanapaswa kuwa ajenda ya kudumu katika ngazi zote za kiutawala kuanzia ngazi ya Kijiji/Mtaa hadi Taifa.

Ili kuwezesha utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa, utaanzishwa utaratibu wa uratibu katika ngazi ya Taifa, Mkoa, Wilaya, Kata na Kijiji/Mtaa na Taasisi. Wajibu na majukumu ya kitaasisi katika muktadha wa utekelezaji wa Mkakati ni kama yalivyoainishwa hapa chini.

## 4.1 Ngazi ya Taifa

Kutakuwa na Kamati mbili za uratibu zitakazoongozwa na Katibu Mkuu Kiongozi. Kamati hizi ni (i) **Kamati ya Taifa ya Uendeshaji** itakayohusisha Taasisi za Umma na Taasisi Zisizokuwa za Kiserikali na (ii) **Kamati ya Taifa ya Kitaalam ya Ushauri** itakayohusisha Taasisi Simamizi za Masuala ya Utawala Bora, Ofisi ya Rais, TAMISEMI na wajumbe wengine watakaoteuliwa kwa wadhifa na umuhimu wao. Sekretariati ya Kamati hii itakuwa chini ya Kitengo cha Uratibu wa Utawala Bora, Ikulu (GGCU).

### 4.1.1 Majukumu ya Kamati ya Taifa ya Uendeshaji

i) Kupokea, kufanya mapitio, kuazimia na kupitisha taarifa za utekelezaji na ufuatiliaji na tathmini za robo mwaka na mwaka za Mkakati;

ii) Kusisitiza umuhimu wa kubadilishana taarifa na uzoefu wa masuala yanayohusu utawala bora;

iii) Kusimamia utekelezaji wa Mkakati katika ngazi zote na kumshauri Katibu Mkuu Kiongozi ipasavyo;

iv) Kuhakikisha taarifa za utekelezaji za Mkakati zinaandaliwa na kuwasilishwa kwa Katibu Mkuu Kiongozi kwa hatua zaidi na kumshauri ipasavyo kuhusu hatua za kuchukuliwa ili kuharakisha utekelezaji wa Mkakati;

v) Kupitia na kuchambua utekelezaji wa Mkakati na kupanga namna ya kuandaa makongamano ya kitaifa kwa lengo la kuharakisha kasi ya utekelezaji;

vi) Kushauri kuhusu sera au jambo lolote linalohusiana na kuboresha utawala bora na ufuatiliaji;

vii) Kuhakikisha Taasisi Simamizi za Masuala ya Utawala Bora zinatekeleza na kuchukua hatua kuhusu utekelezaji wa masuala ya maadili na mapambano dhidi ya rushwa katika maeneo yao; na

viii) Kuanzisha mfumo wa utoaji wa zawadi na adhabu katika utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa.

### 4.1.2 Majukumu ya Kamati ya Taifa ya Kitaalam ya Ushauri

i) Kupokea, kupitia, kushauri, kuazimia na kuidhinisha mipango kazi kutoka katika Wizara, Idara, Wakala, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa hususan sekta za vipaumbele;

ii) Kupokea, kupitia, kuazimia, kutoa ushauri na mapendekezo kuhusu miongozo ya Mkakati wa Awamu ya Tatu;

iii) Kupitia, kuazimia na kushauri kuhusu masuala ya utawala bora;

iv) Kupokea, kuazimia na kutoa mapendekezo kuhusu taarifa za utekelezaji za robo mwaka na mwaka za Taasisi Simamizi za Masuala ya Utawala Bora;

v) Kupokea na kuazimia taarifa za ufuatiliaji na tathmini za utekelezaji wa Mkakati za robo mwaka;

vi) Kuishauri Serikali juu ya mifumo, miongozo ya ubora na mbinu za kuhamasisha na kufuatilia maadili na utawala bora;

vii) Kusisitiza umuhimu wa kubadilishana taarifa na uzoefu wa masuala yanayohusu utawala miongoni mwa Taasisi Simamizi za Masuala ya Utawala Bora; na

viii) Kutoa ushauri elekezi kwa washirika au wadau wengine kuhusu utekelezaji wa Mkakati wa Awamu ya Tatu.

### 4.2 Ngazi ya Mkoa

Kutakuwa na Kamati ya Uratibu wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa ya Mkoa chini ya Uenyekiti wa Mkuu wa Mkoa na wajumbe wake watakuwa ni Kamati ya Ushauri ya Mkoa na Taasisi Simamizi za Masuala ya Utawala Bora. Katibu wa Kamati hii atakuwa ni Katibu Tawala wa Mkoa.

#### 4.2.1 Majukumu ya Kamati ya Uratibu ya Mkoa

(i) Kupokea, kupitia, kuazimia, kuidhinisha na kujumuisha mipango kazi kutoka vikundi, vitengo na Mamlaka za Serikali za Mitaa hususan sekta za kipaumbele;

(ii) Kupokea, kupitia, kuidhinisha, kujumuisha taarifa za utekelezaji za robo mwaka na

mwaka kutoka wilayani, kushauri ipasavyo na kuwasilisha kwa Katibu Mkuu Kiongozi;

(iii) Kuimarisha utaratibu wa kubadilishana taarifa na uzoefu wa utekelezaji wa Mkakati kutoka kwa Taasisi Simamizi za Masuala ya Utawala Bora;

(iv) Kuishauri Serikali kuhusu miongozo mingine ya kiutawala;

(v) Kuratibu, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Mkakati ndani ya Mkoa; na

(vi) Kuanzisha mfumo wa utoaji zawadi na adhabu katika utekelezaji wa Mkakati wa Awamu ya Tatu.

### 4.3 Ngazi ya Wilaya

Kutakuwa na Kamati ya Wilaya ya Uratibu ya Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa itakayokuwa chini ya uenyekiti wa Mkuu wa Wilaya na Wajumbe wake watatoka katika Kamati ya Ushauri ya Wilaya na Taasisi Simamizi za Masuala ya Utawala Bora. Katibu wa Kamati hii atakuwa ni Mkurugenzi wa Halmashauri.

#### 4.3.1 Majukumu ya Kamati ya Uratibu ya Wilaya

(i) Kupokea, kupitia, kuazimia, kuidhinisha na kujumuisha mipango kazi kutoka vikundi, vitengo na Mamlaka za Serikali za Mitaa na taasisi nyingine katika Wilaya;

(ii) Kupokea, kupitia, kuidhinisha, kujumuisha taarifa za utekelezaji za robo mwaka na

mwaka za Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi nyinginezo ndani ya Wilaya, Kata na kuziwasilisha kwa Mkuu wa Mkoa;

(iii) Kuimarisha utaratibu wa kubadilishana taarifa na uzoefu wa utekelezaji wa Mkakati kutoka kwa Taasisi Simamizi za Masuala ya Utawala Bora;

(iv) Kutekeleza miongozo mingine ya utawala bora kama itakavyoelekezwa na Serikali;

(v) Kuratibu, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Mkakati katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi nyingine; na

(vi) Kuanzisha mfumo wa utoaji zawadi na adhabu katika utekelezaji wa Mkakati wa Awamu ya Tatu.

**4.4 Ngazi ya Kata**

Kutakuwa na Kamati ya Kata ya Uratibu wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa itakayokuwa chini ya Uenyekiti wa Afisa Mtendaji wa Kata. Wajumbe wake watatoka katika Kamati ya Maendeleo ya Kata na wengine watakaoalikwa kwa nyadhifa na umuhimu wao. Katibu wa Kamati hii atakuwa ni Afisa Mwandamizi wa Serikali katika Kata husika.

**4.4.1 Majukumu ya Kamati ya Uratibu ya Kata**

(i) Kupokea, kupitia, kuazimia, kuidhinisha na kujumuisha mipango kazi ya Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa kutoka Vijijini na taasisi

nyingine ndani ya Kata;

(ii) Kupokea, kupitia, kuidhinisha, kujumuisha taarifa za utekelezaji za robo mwaka na mwaka za Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa kutoka Vijijini na taasisi zingine ndani ya Kata na kuwasilisha kwa Mkuu wa Wilaya;

(iii) Kutekeleza miongozo mingine ya kiutawala kama inavyoelekezwa na Serikali;

(iv) Kuimarisha utaratibu wa ubadilishanaji taarifa na uzoefu wa masuala yanayohusiana na utawala bora ndani ya Kata;

(v) Kuratibu, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Mkakati katika maeneo ya kiutawala ndani ya Kata; na

(vi) Kupendekeza mfumo wa utoaji zawadi na adhabu katika utekelezaji wa Mkakati.

### 4.5 Ngazi ya Kijiji/Mtaa

Kutakuwa na Kamati ya Kijiji/Mtaa ya Uratibu wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa itakayokuwa chini ya uenyekiti wa Afisa Mtendaji wa Kijiji/Mtaa na Wajumbe wake watatoka katika Halmashauri ya Serikali ya Kijiji/Mtaa na wengine watakaoalikwa kwa nyadhifa na umuhimu wao. Katibu wa Kamati hii atakuwa ni Afisa Mwandamizi wa Serikali katika Kijiji/Mtaa husika.

#### 4.5.1 Majukumu ya Kamati ya Uratibu ya Kijiji/Mtaa

(i) Kupokea, kupitia, kuazimia, kuidhinisha na kujumuisha mipango kazi ya utekelezaji wa

Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa kutoka Vitongoji na taasisi nyingine ndani ya Kijiji/Mtaa;

(ii) Kupokea, kupitia, kuidhinisha, kujumuisha taarifa za utekelezaji za robo mwaka na mwaka za Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa kutoka Vitongoji na taasisi zingine ndani ya Kijiji/Mtaa na kuwasilisha kwa Afisa Mtendaji wa Kata;

(iii) Kubadilishana habari za utekelezaji wa Mkakati kutoka Taasisi Simamizi za Masuala ya Utawala Bora;

(iv) Kutekeleza miongozo mingine ya kiutawala kama inavyoelekezwa na Serikali;

(v) Kuimarisha utaratibu wa ubadilishanaji taarifa na uzoefu wa masuala yanayohusiana na utawala bora ndani ya Kijiji/Mtaa;

(vi) Kuratibu, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Mkakati ndani ya maeneo ya kiutawala ya Kijiji/Mtaa; na

(vii) Kupendekeza mfumo wa utoaji wa zawadi na adhabu katika utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Tatu.

## 4.6 Ngazi ya Taasisi

Ngazi hii itahusisha Taasisi za Umma na Taasisi Zisizo za Kiserikali.

### 4.6.1 Taasisi za Umma

Taasisi za Umma inajumuisha Wizara, Idara za Serikali

Zinazojitegemea, Wakala, Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Mashirika ya Umma.

**4.6.1.1 Majukumu ya Taasisi za Umma**

i) Kuhakikisha kuwa mipango ya kuzuia na kupambana na rushwa kimkakati na kiutendaji inaandaliwa kwa kuzingatia Mpango wa Pili wa Maendeleo wa miaka mitatano (2016/17 - 2020/2021) na Mwongozo wa Mpango wa Bajeti;

ii) Kuhakikisha uzingatiaji wa Sheria, Kanuni, Taratibu na Kanuni za Maadili ya Kitaaluma unafanyika;

iii) Kuendelea kutekeleza hatua za kudhibiti vitendo vya rushwa, utawala usioridhisha na vitendo vya utovu wa maadili;

iv) Kuhakikisha kuwa Kamati za Kudhibiti Uadilifu za kila taasisi zinafanya kazi kwa kuzijengea uwezo na kuzipa fedha za kukidhi mahitaji;

v) Kuimarisha uwazi na uwajibikaji katika kutekeleza shughuli za Serikali;

vi) Kuhakikisha kuwa taasisi husika zina madawati yanayofanya kazi ya kupokea na kushughulikia malalamiko;

vii) Kuhakikisha kuwa kila taasisi ina mkataba wa huduma kwa mteja unaotekelezwa ili kuboresha utoaji wa huduma;

viii) Kuhakikisha kuwa shughuli za Taasisi za

Umma zinazingatia maslahi ya Umma na thamani ya fedha;

ix) Kuimarisha na kuongeza uelewa kuhusu maadili na hatua za kuzuia rushwa miongoni mwa watumishi wa Umma;

x) Kuhakikisha kuanzishwa na kutekelezwa kwa Mkakati wa Upashanaji Habari, Utoaji wa Elimu na Mawasiliano; na

xi) Kuongoza kampeni juu ya maadili ya taifa na mapambano dhidi ya rushwa.

#### 4.6.1.2 Kamati za Taasisi za Umma

Katika kila Taasisi ya Umma kutakuwa na Kamati mbili za uratibu wa Mkakati ambazo ni; **Kamati ya Uongozi ya Usimamizi** itakayokuwa chini ya uenyekiti wa Mkuu wa Taasisi na wajumbe wa Kamati hii watakuwa ni Wakuu wa Idara na Vitengo; na **Kamati ya Kudhibiti Uadilifu** ambayo wajumbe wake watateuliwa na Mkuu wa Taasisi husika.

**a) Majukumu ya Kamati ya Uongozi ya Usimamizi:**

i) Kupokea, kufanya mapitio, kuazimia na kupitisha taarifa za utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini za robo mwaka na mwaka za Mkakati kutoka Kamati ya Kudhibiti Uadilifu na kuwasilisha kwa Katibu Mkuu Kiongozi;

ii) Kutathmini utendaji wa Kamati ya Kudhibiti Uadilifu ili kuongeza kasi na tija ya utekelezaji wa Mkakati;

iii) Kufanya mapitio, kuazimia na kushauri Serikali katika masuala ya Utawala Bora;
iv) Kuishauri Serikali kuhusu miongozo mingine ya kiutawala ili kuimarisha ufanisi katika utendaji na utoaji huduma; na
v) Kuanzisha mfumo wa utoaji wa zawadi na adhabu katika utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa ndani ya Taasisi.

**b) Majukumu ya Kamati ya Kudhibiti Uadilifu:**

i) Kuandaa na kutekeleza Mpango Kazi wa Mapambano Dhidi ya Rushwa wa taasisi husika, kuandaa taarifa za utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini za robo mwaka na mwaka na kuwasilisha kwa Kamati ya Uongozi ya Usimamizi;
ii) Kupokea, kuchambua na kushughulikia malalamiko toka ndani na nje ya Taasisi yanayotokana na ukiukwaji wa maadili. Kamati pia itachukua hatua kwa muda unaofaa au muda usiozidi siku saba kwa malalamiko ya kawaida;
iii) Kushiriki katika kutoa mafunzo kuhusu maadili, utawala bora na mapambano dhidi ya rushwa kwa maafisa wa ngazi za kati, mameneja na watumishi wa kawaida;
iv) Kuhakikisha kanuni za maadili na mienendo ya Utumishi wa Umma kwenye taasisi zinaeleweka kwa ufasaha miongoni mwa

watumishi;

v) Kuhakikisha mafunzo ya awali kuhusu maadili ya Utumishi wa Umma yanatolewa kwa watumishi na waajiriwa wapya kwenye Taasisi husika; na

vi) Kuishauri menejimenti ya taasisi kusimamia na kutekeleza Sheria, Kanuni na Taratibu zilizopo.

### 4.6.2 Taasisi Simamizi za Masuala ya Utawala Bora Kitaifa

Taasisi Simamizi za Masuala ya Utawala Bora Kitaifa zitakuwa na jukumu la kuongoza utekelezaji wa Mkakati wa Awamu ya Tatu kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) Kujenga uwezo wa taasisi na wadau wengine wanaohusika na utekelezaji wa Mkakati;

(ii) Kushiriki katika kuandaa miongozo ya utekelezaji wa Mkakati;

(iii) Kuishauri Serikali na wadau wengine juu ya namna bora ya kutekeleza Mkakati wa Awamu ya Tatu;

(iv) Kuongoza kampeni za kuhamasisha maadili ya kitaifa na utekelezaji wa hatua za kudhibiti rushwa nchini;

(v) Kuwezesha uandaaji wa Sera ya Maadili ya Taifa;

(vi) Kuwezesha utekelezaji wa Sheria ya Watoa Taarifa na Mashahidi ya Mwaka 2015 ili kusaidia utekelezaji wa Mkakati;

(vii) Kushiriki pamoja na wadau wengine katika mijadala ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa kuhusu utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa; na

(viii) Kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Mkakati wa Awamu ya Tatu.

**4.6.3 Taasisi Zisizokuwa za Kiserikali**

Taasisi Zisizokuwa za Kiserikali zinajumuisha Wabia wa Maendeleo, AZAKI, Sekta Binafsi, Vyama vya Siasa na Vyombo vya Habari.

**4.6.3.1 Majukumu ya Wabia wa Maendeleo**

(i) Kuwezesha utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Tatu kwa kutoa fedha na utaalamu kwa Serikali na AZAKI;

(ii) Kusaidia kufanyika kwa tathmini huru ya utekelezaji wa Mkakati wa Awamu ya Tatu; na

(iii) Kushiriki katika mijadala na Serikali pamoja na wadau wengine juu ya utekelezaji wa Mkakati wa Awamu ya Tatu.

**4.6.3.2 Majukumu ya Asasi za Kiraia (Taasisi za Kidini, Taasisi za Kijamii, Vyama vya Wafanyakazi)**

(i) Kuunda umoja na ushirika wa AZAKI na Serikali ili kuwezesha utekelezaji wa Mkakati;

(ii) Kuandaa na kutekeleza mpango kazi unaotekelezeka katika maeneo ya mamlaka zao;

(iii) Kushiriki katika kuanzisha na kuhamasisha elimu ya maadili ya Taifa;
(iv) Kushiriki katika mijadala na mazungumzo na Serikali pamoja na wadau wengine kuhusu utekelezaji wa Mkakati wa Awamu ya Tatu;
(v) Kuimarisha kiwango cha uwazi na uwajibikaji katika kutekeleza majukumu yao;
(vi) Kushiriki katika kampeni za maadili ya Taifa na Utawala Bora;
(vii) Kufanya utafiti na mafunzo kuhusiana na rushwa, maadili na utawala bora;
(viii) Kuishauri Serikali kuhusu masuala ya maadili na mapambano dhidi ya rushwa ikiwemo ushiriki katika kuandaa Sera na kuzitekeleza; na
(ix) Kuhamasisha na kutekeleza Mkakati wa Upashanaji Habari, Elimu na Mawasiliano ya Mkakati wa Awamu ya Tatu.

**4.6.3.3 Majukumu ya Sekta Binafsi**

(i) Kuingiza hatua za udhibiti wa rushwa na maadili katika mipango kazi yao;
(ii) Kuandaa na kutekeleza mfumo wa uzingatiaji wa maadili katika biashara;
(iii) Kuhakikisha kuwa Sheria, Kanuni na Taratibu zinazohusu maadili ya biashara zinazingatiwa;
(iv) Kujiunga na kutekeleza makubaliano ya maadili ya kibiashara na miongozo ya kimataifa;
(v) Kuimarisha uwazi na uwajibikaji katika

utekelezaji wa majukumu yao;

(vi) Kufanya utafiti na mafunzo kuhusiana na rushwa, maadili na utawala bora;

(vii) Kuimarisha ushirikiano kati ya Sekta ya Umma na Binafsi katika mapambano dhidi ya rushwa; na

(viii) Kuandaa mipango kazi kwa ajili ya utekelezaji wa Mkakati katika maeneo yao.

**4.6.3.4 Majukumu ya Vyama vya Siasa**

(i) Kuhakikisha uwepo wa uwazi na maadili katika michakato ya uchaguzi ili kuimarisha demokrasia katika chaguzi;

(ii) Kushiriki na kuonesha utashi wa dhati wa kuimarisha maadili na kuyasimamia miongoni mwa wanachama wao;

(iii) Kuhakikisha kuwa Sheria ya Gharama za Uchaguzi Na.6/2010 inazingatiwa wakati wote;

(iv) Kujenga uwezo wa wanachama na jamii wa kudhibiti vitendo vya rushwa na utovu wa maadili;

(v) Kuingiza malengo ya udhibiti wa rushwa na maadili katika Katiba za Vyama vya Siasa na Ilani za Uchaguzi; na

(vi) Kushirikiana na Serikali na Wadau wengine katika mijadala na mazungumzo kuhusu utekelezaji wa Mkakati wa Awamu ya Tatu.

#### 4.6.3.5 Majukumu ya Vyombo vya Habari

i) Kuhakikisha kuwa maadili ya taaluma ya habari yanazingatiwa;

ii) Kukuza na kufuatilia maadili ya jamii kitaifa kama njia ya kupambana na rushwa na makosa mengine nchini;

iii) Kuhamasisha na kutekeleza hatua za kudhibiti maadili na rushwa katika vyombo vya habari;

iv) Kujenga uwezo wa Wanahabari juu ya maadili, rushwa na utawala bora; na

v) Kuhamasisha na kutangaza Mkakati wa Awamu ya Tatu kwa umma.

# SURA YA TANO

# UFUATILIAJI NA TATHMINI

## 5.0 Utangulizi

Ufuatiliaji ni utaratibu unaofanyika katika kipindi chote cha utekelezaji wa kazi ili kuhakikisha kuwa zinatekelezwa kama zilivyopangwa. Ufuatiliaji hufanyika katika matumizi ya rasilimali kwa kulinganisha na kazi zilizofanyika kwa lengo la kutathmini utekelezaji, kubainisha mapungufu, kutoa mrejesho kwa watekelezaji na kurekebisha mapungufu ya kiutendaji yaliyojitokeza kabla hayajasababisha ucheleweshaji wa utekelezaji.

Tathmini hufanyika kupima matokeo ya kazi zilizokamilika au zinazoendelea kulingana na malengo yaliyowekwa. Aidha, inaunganishwa na matokeo ya mwisho yakilinganishwa na ya awali. Pia, kwa kawaida tathmini hufanyika katika kipindi cha kati au mwisho wa utekelezaji.

Ufuatiliaji na Tathmini utafanyika kupitia Mpango wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Tatu ulioandaliwa na ambao taasisi zitakazotekeleza zitapaswa kuzingatia mfumo huo ili kuhakikisha utekelezaji wa Mkakati unafanyika kwa ufanisi na matokeo yake kupimika.

Ufuatiliaji wa Mkakati utafanyika katika ngazi zote za utekelezaji na wahusika wakuu wa kazi hii ni Kamati

ya Taifa ya Uendeshaji, Kamati ya Taifa ya Kitaalam ya Ushauri, Kitengo cha Uratibu wa Utawala Bora, Ofisi ya Rais Ikulu, Kamati za Uratibu wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa za Mikoa, Wilaya, Kata, Kijiji/Mtaa, Kamati za Kudhibiti Uadilifu za Taasisi na Kamati za Uongozi za Usimamizi. Hivyo, kila mdau wa utekelezaji anatakiwa kuandaa na kutekeleza Mpango wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Mkakati wa Awamu ya Tatu.

## 5.1 Madhumuni ya Mpango wa Ufuatiliaji na Tathmini

Madhumuni makuu ya Mpango wa Ufuatiliaji na Tathmini ni kama ifuatavyo:

i) Kuweka mikakati inayoeleweka ya ufuatiliaji na tathmini itakayowezesha ukusanyaji wa takwimu kwa mpangilio ili zitumike katika kupima mafanikio na kubaini mabadiliko katika mchakato wa utekelezaji;

ii) Kuhamasisha uwepo wa ubia na kuwaunganisha wadau katika ngazi mbalimbali ili kuleta ufanisi katika ufuatiliaji na tathmini na kutoa mrejesho;

iii) Kuboresha ubadilishanaji, usambazaji na matumizi ya takwimu zilizopatikana kwa ajili ya mipango na hatua za baadaye;

iv) Kuwajengea uwezo wadau wa utekelezaji wa Mkakati wa Awamu ya Tatu katika kukusanya, kuchambua na kutumia takwimu za ufuatiliaji na tathmini;

v) Kufuatilia mafanikio ya Mkakati wa Awamu ya Tatu pamoja na kubainisha njia sahihi za utekelezaji ili kuufanya Mkakati kuwa endelevu; na
vi) Kufanya utafiti utakaowezesha kuandaa vigezo vya kupima hali ya rushwa kitaalamu.

## 5.2 Muundo wa Ufuatiliaji na Tathmini

Kama ilivyoelezwa hapo juu, ufuatiliaji na tathmini utafanyika kupitia mpango madhubuti wa Ufuatiliaji na Tathmini. Mpango huu umegawanyika katika sehemu kuu tano kama ifuatavyo:

**i)** **Sehemu ya kwanza** ni utangulizi wa Mpango;
**ii)** **Sehemu ya pili** inahusu mfumo wa matokeo ya Mkakati wa Awamu ya Tatu na vigezo vikuu vya upimaji;
**iii)** **Sehemu ya tatu** inaelezea vyanzo vikuu vya takwimu kwa ajili ya Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini;
**iv)** **Sehemu ya nne** inaelezea taarifa kuu tarajiwa na utaratibu wake wa kuzisambaza; na
**v)** **Sehemu ya tano** inaelezea mfumo wa kimpangilio kuhusu utekelezaji wa Mpango madhubuti wa Ufuatiliaji na Tathmini na Viashiria.

## 5.3 Mfumo wa Viashiria vya Upimaji Matokeo

Mfumo wa Matokeo ya Utekelezaji wa Mkakati wa Awamu ya Tatu utaandaliwa ili kubainisha na kutenganisha viashiria vikuu muhimu vya upimaji vya kitaifa na vyanzo vyake. Mfumo utaandaliwa kwa kuzingatia Mwongozo

wa utekelezaji wa Mkakati wa Awamu ya Tatu na ushauri kutoka kwa wadau. Vigezo na Viashiria vya upimaji vitaonesha aina ya taarifa ambazo zitakusanywa kwa kutumia Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Mkakati wa Awamu ya Tatu.

### 5.3.1 Mfumo wa Matokeo na Uchaguzi wa Viashiria vya Upimaji

Mfumo wa Upimaji wa Matokeo na Viashiria vya Upimaji vitatokana na Mpango Kazi, malengo, mbinu na matokeo ya Mkakati wa Awamu ya Tatu kama ifuatavyo:

i) Kuweka kipaumbele kwa sekta zenye ushawishi wa rushwa;
ii) Kuimarisha utekelezaji wa sheria, usimamizi na utoaji wa motisha katika mapambano dhidi ya rushwa;
iii) Kuimarisha na kuwezesha umma kushiriki kudai haki na uwajibikaji wa Serikali;
iv) Kuimarisha elimu ya maadili na mapambano dhidi ya rushwa kupitia Mkakati wa Habari, Elimu na Mawasiliano;
v) Kuimarisha ubia baina ya Asasi za Kiraia, Serikali, Bunge, Mahakama, Vyama vya Siasa, Vyombo vya Habari, Sekta Binafsi na Wabia wa Maendeleo katika mapambano dhidi ya rushwa.
vi) Kuimarisha na kuboresha mifumo ya utawala wa vyombo vya utoaji wa haki;
vii) Kuimarisha na kuzijengea uwezo Taasisi

Simamizi za Masuala ya Utawala Bora, Kamati za Kudhibiti Uadilifu na Kamati za Uratibu wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa za Wizara, Idara za Serikali Zinazojitegemea, Wakala wa Serikali, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Bunge, Mahakama na Asasi Zisizokuwa za Kiserikali;

viii) Kuweka mkazo katika matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma;

ix) Kukuza uwazi na uwajibikaji katika utekelezaji wa shughuli za Umma na Binafsi;

x) Kuingiza elimu ya maadili na masuala ya rushwa kwenye mitaala na mifumo ya elimu kwa shule za Msingi, Sekondari, Vyuo vya Elimu ya Juu wakiwemo vijana walio nje ya mfumo rasmi wa elimu; na

xi) Kuimarisha uratibu wa ufuatiliaji na tathmini katika utekelezaji wa Mkakati nchini.

Taarifa na takwimu kutoka katika Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini zitatokana na taarifa za utekelezaji, taarifa za matokeo ya kazi za utafiti pamoja na tathmini ya utekelezaji ya kila taasisi kama inavyooneshwa kwa muhtasari katika Jedwali Na.1 hapa chini.

## Jedwali Na 1: Muhtasari wa Upimaji Matokeo na Vyanzo vya Takwimu

| Na | Chanzo cha Takwimu | Nyenzo za Ukusanyaji Takwimu | Muda wa Utoaji Taarifa | Taasisi Husika | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|
| **A: UTAFITI NA UCHAMBUZI** | | | | | |
| 1 | Utafiti kwa umma kuhusu matokeo ya Mkakati (GPIS) | Utafiti & Mapitio ya Taarifa mbalimbali | Kipindi cha kati na mwisho cha utekelezaji | Kitengo Utawala Bora, TAKUKURU, Taasisi za Utafiti | Kama itaka-vyokubaliwa |
| 2 | Mfumo wa ufuatiliaji wa Malalamiko ya Umma (PCTS) | Utafiti & Mapitio ya Taarifa mbalimbali | Kila robo mwaka | Kitengo Utawala Bora, Utumishi-(Dep), BRELA, Sekretarieti ya Maadili | Kama itaka-vyokubaliwa |
| 3 | Taarifa toka kwa wakala za uchunguzi kuhusu kesi za hongo, rushwa, udanganyifu na vitendo vinginevyo visivyo vya kimaadili (IARs) | Utafiti & Mapitio ya Taarifa mbalimbali | Kila robo mwaka | Waajiri, Polisi, TAKUKURU, THBUB, Mdhibiti wa Hesabu za Serikali, Sekretarieti ya Maadili na Mamlaka ya Mapato Tanzania | Kama itaka-vyokubaliwa |
| 4 | Taarifa za uwajibikaji za fedha za umma (PFARs) | Mapitio ya Taarifa mbalimbali | Kila mwaka | Mdhibiti wa Hesabu za Serikali, Hazina, Tamisemi, Taasisi za Utafiti | Kama itaka-vyokubaliwa |

| Na | Chanzo cha Takwimu | Nyenzo za Ukusanyaji Takwimu | Muda wa Utoaji Taarifa | Taasisi Husika | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|
| 5 | Utafiti wa matokeo ya Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji Awamu ya III (OS) | Utafiti & Mapitio ya Taarifa mbalimbali | Kipindi cha kati na mwisho cha utekelezaji | Kitengo cha Utawala Bora, TAKUKURU | Kama itaka-vyokubaliwa |
| 6 | Taarifa za Manunuzi ya Umma kuhusu thamani ya fedha (PPRs) | Utafiti & Mapitio ya Taarifa mbalimbali | Kila mwaka | Wizara, Idara Zinazo-jitegemea, Wakala, TAMISEMI na Taasisi za Utafiti | Kama itaka-vyokubaliwa |
| 7 | Kupata maoni kutoka kwa Wananchi kuhusu Jitihada za Serikali katika mapambano dhidi ya Rushwa | Utafiti & Mapitio ya Taarifa mbalimbali | Kila mwaka | TAKUKURU, Kitengo cha Utawala Bora, Sekretarieti ya Maadili, Utumishi-DEP, TAMISEMI, Taasisi za Kitafiti | Kama itaka-vyokubaliwa |
| 8 | Kupata maoni ya Wananchi kuhusu hali na mwenendo wa rushwa | Utafiti & Mapitio ya Taarifa mbalimbali | Kila mwaka | TAKUKURU, Kitengo cha Utawala Bora, Sekretarieti ya Maadili, Utumishi-DEP, TAMISEMI, Taasisi za Kitafiti | Kama itaka-vyokubaliwa |

| Na | Chanzo cha Takwimu | Nyenzo za Ukusanyaji Takwimu | Muda wa Utoaji Taarifa | Taasisi Husika | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|
| 9 | Kupata maoni ya Wananchi kuhusu hali na mwenendo wa rushwa katika Biashara | Utafiti & Mapitio ya Taarifa mbalimbali | Kila mwaka | TAKUKURU, Kitengo cha Utawala Bora, Sekretarieti ya Maadili, Utumishi-DEP, TAMISEMI, Taasisi za Kitafiti | Kama itaka-vyokubaliwa |
| 10 | Kupata maoni ya Wananchi kuhusu hali na mwenendo wa rushwa kwenye Vyama Siasa | Utafiti & Mapitio ya Taarifa mbalimbali | Kila mwaka | TAKUKURU, Kitengo cha Utawala Bora, Sekretarieti ya Maadili, Utumishi-DEP, TAMISEMI, Taasisi Za Kitafiti | Kama itaka-vyokubaliwa |
| **B: FOMU ZA UFUATILIAJI WA UTEKELEZAJI WA MKAKATI (QAIMF)** | | | | | |
| 1 | Fomu ya ufuatiliaji wa kazi za robo mwaka za Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa utekelezaji Awamu ya Tatu. | Utafiti & Mapitio ya Taarifa mbalimbali | Kila robo mwaka | Waratibu Kutoka Wizara, Idara Zinazo-jitegemea, Wakala, TAMISEMI na Taasisi za Utafiti | Kama itaka-vyokubaliwa |

## 5.4 Usambazaji na Matumizi ya Taarifa

Madhumuni ya Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Tatu ni kuwawezesha wadau kupata taarifa na takwimu sahihi ambazo zitatumika kwa ajili ya kuchukua hatua, kupanga na kuboresha utekelezaji wa kazi zao. Mpango huo utabainisha wadau muhimu, mahitaji yao, taarifa nyinginezo muhimu na jinsi zitakavyosambazwa kwa wadau.

## 5.5 Taarifa kwa Wadau

Taarifa za Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Mkakati wa Awamu ya Tatu zitatumiwa na wadau ambao miongoni mwao ni pamoja na Serikali, Bunge, Mahakama, Vyama vya Siasa, Watafiti na Wanazuoni, Asasi Zisizo za Kiserikali, Umma na Wabia wa Maendeleo.

## 5.6 Utoaji wa Taarifa za Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji Awamu ya Tatu

Kitengo cha Uratibu wa Utawala Bora, Ofisi ya Rais, Ikulu kitaandaa na kusambaza taarifa zifuatazo:

i) Taarifa za Utafiti wa Msingi za Mkakati ;
ii) Taarifa za Utekelezaji za Robo Mwaka za Mkakati; na
iii) Taarifa ya Mwaka ya Utekelezaji ya Mkakati.

## 5.7 Mchakato wa Utoaji Taarifa

### 5.7.1 Vyanzo vya Taarifa

Kwa kutumia nyenzo za ukusanyaji wa takwimu, taarifa itaandaliwa kwa kutumia taarifa za upili zilizopo na nyinginezo za ziada kuhusu hali ilivyo sasa kabla ya utekelezaji haujaanza. Taasisi zinazotekeleza Mkakati zitakuwa ndiyo vyanzo vikuu vya taarifa ambapo watatakiwa kuwasilisha taarifa hizi Kitengo cha Uratibu wa Utawala Bora- Ikulu kila robo mwaka ili kuwezesha mchakato wa uandaaji wa taarifa ya jumla ya utekelezaji wa Mkakati.

### 5.7.2 Taarifa za Utekelezaji za Robo Mwaka

Katika ngazi ya Taifa, Kitengo cha Uratibu wa Utawala Bora, Ofisi ya Rais, Ikulu kitaandaa taarifa za utekelezaji za Mkakati wa Awamu ya Tatu za robo mwaka. Taarifa itatolewa kwa njia ya takwimu kuonesha wigo wa rasilimali na matokeo ya vigezo vya upimaji vilivyomo katika mfumo wa upimaji wa matokeo wa Mkakati ili kuwapa wadau taarifa ya kazi zilizotekelezwa katika kipindi cha robo mwaka. Takwimu hizi zitawasaidia wadau kubaini mapungufu na hivyo kupanga vyema malengo yao kwa kutumia rasilimali zilizopo ili kuleta ufanisi katika utekelezaji wa Mkakati.

### 5.7.3 Taarifa ya Mwaka ya Utekelezaji

Madhumuni ya taarifa ya mwaka ya utekelezaji ya Mkakati wa Awamu ya Tatu ni kutoa matokeo na jitihada za utekelezaji wa Mkakati. Taarifa hii italenga maeneo

ya matokeo makubwa yaliyobainishwa katika Mpango wa Ufuatiliaji na Tathmini, Vigezo Vikuu vya Upimaji vya Mkakati wa Awamu ya Tatu na taarifa nyinginezo muhimu.

### 5.7.4 Taarifa ya Tathmini ya Upimaji wa Matokeo

Taarifa hii itaandaliwa katika kipindi cha kati na cha mwisho cha utekelezaji wa Mkakati na itakuwa na takwimu zote za viashiria vya upimaji vilivyoandaliwa kwa kuzingatia Mwongozo wa Ufuatiliaji na Tathmini. Takwimu za viashiria zitawasilishwa kwa mfumo wa majedwali. Majedwali yatatumika kutoa taarifa za takwimu za viashiria za kuanzia, malengo na kipindi ambacho taarifa zitatolewa ili kulinganisha vipindi vya utekelezaji.

### 5.7.5 Uchambuzi na Uunganishaji wa Takwimu

Utaandaliwa Mfumo wa Takwimu na Kanzidata kwa ajili ya utekelezaji wa Mkakati wa Awamu ya Tatu utakaosaidia uandaaji wa taarifa. Zana na nyenzo mbalimbali zitatumika ili kuunganisha na kufanya uchambuzi na baadaye kutengeneza chati, grafu na njia nyinginezo za uwasilishaji wa takwimu kwa urahisi zaidi zitakazoeleweka vyema kwa kila Mdau.

### 5.7.6 Uidhinishwaji na Usambazaji wa Taarifa

Taarifa ya utekelezaji wa Mkakati itaandaliwa na Kitengo cha Uratibu wa Utawala Bora, Ofisi ya Rais, Ikulu na kuidhinishwa na Katibu Mkuu Kiongozi ili zisambazwe kwa wadau.

### 5.7.7 Taarifa kwa Wadau

Ili kuimarisha ushirikishwaji wa Wadau, Kitengo cha Uratibu wa Utawala Bora kitaandaa jukwaa la Kitaifa la Mapambano Dhidi ya Rushwa ili kujadili taarifa za nusu mwaka na mwaka za Ufuatiliaji na Tathmini ya Mkakati. Kwa mawasiliano ya karibu na wadau, orodha ya anuani zao itaandaliwa na kuhuishwa kila inapohitajika.

## 5.8 Mfumo wa Mpangilio wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Mkakati wa Awamu ya Tatu

### 5.8.1 Uratibu wa utekelezaji wa Mkakati wa Awamu ya Tatu

Kitengo cha Uratibu wa Utawala Bora, Ofisi ya Rais, Ikulu kitaendelea na jukumu lake la kuratibu utekelezaji wa kazi za mapambano dhidi ya rushwa zinazofanywa na wadau wengine kama vile TAKUKURU, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Kuhusu ufuatiliaji na tathmini, Kitengo kitafanya kazi kwa karibu na watekelezaji wa Mkakati wa Awamu ya Tatu hasa Kamati za Kudhibiti Uadilifu, Kamati za Uratibu wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa za Mikoa, Wilaya, Kata na Kijiji/Mtaa huku jitihada zikifanyika kushauriana na Asasi Zisizo za Kiserikali ili kuwa sehemu ya mchakato huu. Kitengo cha Uratibu wa Utawala Bora kitatumia taarifa za ufuatiliaji na tathmini kutekeleza mapendekezo ya kisera na kuziimarisha taasisi zinazofanya vibaya katika jitihada za mapambano dhidi ya rushwa.

Ufuatiliaji wa utekelezaji utaongozwa na mpango kazi wa Mkakati wa Awamu ya Tatu wa kila taasisi utakaokuwa na kazi, vigezo vya upimaji na malengo yenye kueleweka. Hivyo, katika ngazi ya Taifa Katibu Mkuu Kiongozi kupitia Kitengo cha Uratibu wa Utawala Bora, Ofisi ya Rais, Ikulu atasimamia kazi za ufuatiliaji na tathmini na katika ngazi ya Taasisi, Wakuu wa Taasisi za Umma na Binafsi watakuwa na jukumu hili kupitia Kamati za Kudhibiti Uadilifu na Kamati za Uongozi za Usimamizi.

### 5.8.2 Mfumo wa Kanzidata wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji wa Awamu ya Tatu

Ili kuwezesha mfumo wa ubadilishanaji wa taarifa, Kitengo cha Uratibu wa Utawala Bora kitaanzisha mfumo wa takwimu na kanzidata wa ufuatiliaji na tathmini. Itifaki ya kanzidata ya ufuatiliaji na tathmini itaandaliwa ili kuhakikisha takwimu zinahuishwa kila mara na kwa wakati. Itifaki itabainisha wakati gani wa kuhuisha takwimu, takwimu zinazopaswa kuhuishwa, mhusika anayeruhusiwa kuzifanyia marekebisho na utaratibu wa utunzaji wa takwimu.

Inakusudiwa pia takwimu hizi zipatikane mtandaoni kupitia wavuti wa Mkakati wa Awamu ya Tatu baada ya kuanzishwa. Hii itawezesha jamii kutumia fursa ya huduma za mtandao ili kufuatilia utekelezaji wa Mkakati. Kitengo cha Uratibu wa Utawala Bora pia kitahakikisha kanzidata za ufuatiliaji na tathmini zinajumuishwa katika

mifumo mingine ya Serikali ya upatikanaji wa taarifa.

Taarifa za Ufuatiliaji na Tathmini zitawasilishwa kwenye Kamati ya Taifa ya Uendeshaji na Kamati ya Taifa ya Kitaalam ya Ushauri kwa kuchambuliwa na kutolewa maazimio.

### 5.8.3 Bajeti na Mpango Kazi wa Ufuatiliaji na Tathmini

Ili Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini uweze kufanya kazi, taasisi zinatakiwa ziandae mipango kazi na kutenga fedha katika bajeti zao kwa ajili ya utekelezaji.

## SURA YA SITA

## MWONGOZO WA UANDAAJI WA MPANGO KAZI WA UTEKELEZAJI WA MKAKATI WA TAIFA DHIDI YA RUSHWA AWAMU YA TATU

### 6.0 Utangulizi

Rushwa ni moja ya vyanzo vikuu vya matatizo ya kiuchumi na kijamii nchini. Imekuwa tishio katika utendaji wa mifumo ya kisiasa, mshikamano wa kijamii na maendeleo ya Nchi. Hali ilivyo sasa inahitaji jitihada za pamoja miongoni mwa wadau muhimu kwa kutekeleza Mkakati madhubuti ulioandaliwa sambamba na mikakati mingine jumuishi ya kitaifa.

Aidha, katika kurahisisha utekelezaji wa Mkakati huu, Serikali imeandaa Mwongozo wa Utekelezaji wenye lengo la kuwaongoza watekelezaji wa Mkakati kufahamu masuala muhimu ya kuzingatia ili Mkakati utekelezwe kwa ufanisi. Mambo muhimu yanayohitajika katika utekelezaji wa Mkakati ni pamoja na uandaaji wa nyaraka na uteuzi wa wajumbe wa Kamati zifuatazo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| i) | Mpango Kazi | - | Wadau wote |
| ii) | Kamati ya Uratibu ya Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa | - | Ngazi ya Mkoa, Wilaya, Kata, Kijiji/Mtaa |
| iii) | Kamati za Kudhibiti Uadilifu | - | Wadau wote |

| | | | |
|---|---|---|---|
| iv) | Kamati ya Uongozi ya Usimamizi | - | Ngazi ya Taasisi |
| v) | Kamati ya Taifa ya Uendeshaji | - | Kitengo cha Uratibu wa Utawala Bora-Ikulu |
| vi) | Kamati ya Taifa ya Kitaalam ya Ushauri | - | Kitengo cha Uratibu wa Utawala Bora-Ikulu |
| Vii) | Mpango wa Ufuatiliaji na Tathmini | - | Wadau wote |
| viii) | Utoaji wa taarifa kupitia fomu Na. 5.1 na 5.2 | - | Wadau wote |

## 6.1 Mipango Kazi

Taasisi za Umma zikiwemo Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatakiwa kuandaa na kutekeleza mipango kazi inayozingatia kazi kuu za taasisi, vipaumbele vya Taifa vya kuzuia na kupambana na rushwa, malengo mahsusi ya Mkakati katika muktadha wa mazingira yao. Sekta Binafsi na Asasi za Kiraia kwa upande wake zitahamasishwa ili nazo ziandae mpango kazi wa utekelezaji wa Mkakati katika maeneo ya mamlaka yao. Mipango kazi hii inapaswa kuzingatia hatua mahsusi kama zilivyoainishwa katika Jedwali Namba 2.

## 6.2 Lengo na Mikakati ya Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji Awamu ya Tatu

